epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Aprili 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581644
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**BRANTHWAITE HATAKI 'KELELE'**

# Maafa ya mvua

## • Apishana na gari lake likisombwa na maji akitoka ofisini; uokoaji waanza Rufiji...

*Endelea ukurasa 2 &3*





Mwonekano wa juu wa eneo la Kisongo, kata ya Matevesi, wilayani Arumeru, mkoani Arusha, baada ya mvua kubwa kunyesha usiku wa kuamkia jana na kusababisha mafuriko yaliyofanya uharibifu wa vitu mbalimbali. Picha ndogo: Magari na pikipiki yaliyoharibiwa. **PICHA ZOTE: GETRUDE MPEZYA**

**Bomoabomoa** nyumba 2,155 kurindima Bonde la Msimbazi UKURASA 4

**Aliyetumbuliwa** kisa vipimo vya corona arejeshwa kazini baada ya miaka 4 UKURASA 4

**Mahakama:** Sheria ya Vileo inakinzana na Katiba ya Z'bar UKURASA 17

KILIO CHA KIKOKOTOO

## TUCTA yapeleka hoja kwa Rais kupitia barua

UKURASA 2



## Hatimaye DP World yaanza kazi Bandari D'Salaam

UKURASA 19

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA SC HASIRA LIGI KUU BARA** UK.24

**KATUNI** UK.6



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania, Roghat Robert akifundisha somo la uandishi wa taarifa binafsi (CV) na barua za kiofisi kwa vijana wanachama wa shirika hilo, mjini Tabora jana, ili kuwarahisishia wakati wa kutafuta ajira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KILIO CHA KIKOKOTOO

# TUCTA wamwandikia barua Rais Samia

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), limemwandikia barua Rais Samia Suluhu Hassan, kuelezea changamoto mbalimbali zinazokabili wafanyakazi, kikiwamo kilio dhidi ya kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu, nyongeza ya mishahara na bima ya afya.

Hatua hiyo ilibainishwa jana na Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusu maandalizi ya sherehe za Mei Mosi ambazo mwaka huu zimepangwa kufanyika mkoani Arusha.

Alisema kuwa kupitia barua yao hiyo kwa Rais, wameeleza changamoto mbalimbali ambazo wafanyakazi wanakabiliana nazo zinazojumuisha pia malimbikizo ya fedha za likizo ili serikali izifanyie kazi kuelekea sherehe za Mei Mosi.

"Tumemwandikia barua Mheshimiwa Rais, yapata mwezi mmoja uliopita. Tumeainisha changamoto zote za wafanyakazi. Kwahiyo, tunatarajia serikali itafanyia kazi changamoto hizo na tunasubiri majibu ya barua yetu," alisema.

Rais huyo wa TUCTA alisema shirikisho hilo linapambana kuhakikisha mstaafu anapata mafao mazuri na wakati huohuo mifuko ya hifadhi ya jamii nayo inabaki salama kwa kuwa wanatambua ikitoa fedha nyingi nalo ni tatizo. Ndicho kiini cha kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu.

Alisema mifuko ya pensheni ni mali ya wafanyakazi, si ya serikali, hivyo ni lazima shirikisho lihakikishe linapopambania ongezeko la mafao, linaangalia pia ustawi wa mifuko kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

"Haikuwa kazi rahisi, tumepambana sana kupandisha kikokotoo kutoka asilimia 25 wakati wa utawala wa awamu ya tano mpaka kufikia asilimia 33. Kwahiyo, ingawa tunapenda kuona kinaongezeka, lakini lazima tuangalie na uhai wa mifuko hii" alisema.

"ILO (Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa) wanaiangalia hii mifuko kwa jicho la karibu sana na mimi kila mwaka lazima nipeleke ripoti huko.

"Wanataka kujua uhai wa mifuko kwa sababu hii ni mali ya wanachama, si mali ya serikali. Lazima wananchi wafahamu hili," alisema Nyamhokya.

Kuhusu nyongeza ya mishahara, Rais wa TUCTA alisema serikali ilitekeleza ahadi yake ya kuongeza mishahara iliyoitoa Mei Mosi, 2023 ingawa wafanyakazi wengi walilalamika kuwa ni nyongeza ndogo kulinganisha na hali ya gharama za maisha.

"Kwa miaka kama saba hakukuwa na nyongeza ya mishahara, hivyo wafanyakazi walipotangaziwa kutakuwa na nyongeza ya mishahara, walikuwa na matarajio makubwa sana, wakadhani itakuwa kubwa, sasa walipoona wengine wamepata Sh. 20,000 wakashangaa sana!" alisisitiza.

Aliwataka wafanyakazi nchini kuendelea kuchapa kazi kwa kuwa shirikisho linafahamu changamoto zao na limekuwa linafanya mawasiliano ya mara kwa mara na serikali kwa ajili ya kupata majibu ya changamoto hizo.

Katika sherehe za Mei Mosi zilizofanyika kitaifa mwaka jana mkoani Morogoro, Rais Samia aliahidi kuwa nyongeza ya mishahara iliyokwua imesitishwa kwa muda mrefu, inarejeshwa na serikali na itakuwa inatolewa kila mwaka.

Pia aliahidi serikali itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa serikali na wale wa sekta binafsi, ili kuwe na ajira zenye usalama na zenye staha kwa wote.

Tangu kuanza kutumika kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu mwaka jana, kumekuwa na ukosoaji dhidi ya kanuni hizo za kutoa mafao kutoka makundi mbalimbali, wakiwamo wastaafu wenyewe.

Mwanzoni mwa juma hili, baadhi ya wabunge walikipinga vikali kikokotoo hicho wakati wakichangia mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2024/25.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, ni miongoni mwa walioitaka serikali kurejea katika kikokotoo cha zamani cha asilimia 50 na kuachana na kipya cha asilimia 33.

"Nimepitia kanuni mbalimbali kama vile hii ya mwezi Mei 2022 ya Agosti 12, 2018, kanuni ya SCRA 2017 na 2018 pia na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge 2017 pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani ya 2017.

"Kikokotoo kilichokuwapo hadi mwaka 2014 kilikuwa ni kikokotoo kizuri na ndicho Watanzania wengi wanakitaka, chenyewe kilikuwa kimechukua asilimia 50 ambacho kilionesha miaka ya kuishi baada ya kustaafu kuwa ni 15 na nusu, pia kilichukua mshahara wa mwisho wa mfanyakazi ambao mara nyingi huwa ni mkubwa," alisema Gambo.

Vilevile, alisema kwa kikokotoo kipya kimepunguza mafao kutoka 1/540 hadi 1/580 pia wamechukua wastani wa miaka 10, wakitafuta miaka mitatu iliyo bora ambapo kwa kawaida lazima mshahara utafupungua na kuathiri mafao, pia miaka ya kuishi imepunguzwa hadi 12, kitu alichodai si sahihi.

"Nimechukua mfano, sampuli ya mishahara na nimefanya mahesabu kwa mtumishi ambaye anastaafu akiwa na mshahara Sh. 800,000. Kwa kikokotoo cha kabla ya Julai 2014 katika mfuko wa LAPF na PSPF alikuwa anapata Sh. 57,466,666 na kwa kikokotoo cha sasa anapata Sh. 28,675,862 tofauti ya Sh. milioni 29,190,804. Kwa mwezi atapata Sh. 401,000 kwa kikokotoo cha zamani na cha sasa atapata 388,137," alifafanua mbunge huyo.

# Mvua yaleta maafa

**Na Waandishi Wetu,**
ARUSHA

HAKUNA kilichobaki. Ndivyo inavyoweza kuelezwa, baada ya mvua iliyonyesha kwa saa saba katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, kusababisha maafa ya mafuriko yaliyosomba magari, vyakula na vyombo vya ndani, mashamba na kuacha watu bila makazi, huku mtoto mwaka mmoja na nusu, akiokolewa kwa kutupwa juu ya bati.

Wafanyabiashara wamepoteza mali, bidhaa za ujenzi madukani, maghala ya kuhifadhia mazao na pembejeo za kilimo baada ya kusombwa na mafuriko hayo.

Baadhi ya madaraja eneo hilo la Kisongo, Kata ya Mateves, yamejaa miti na mawe makubwa yaliyotokea milimani. Magari yaliyokuwa yameegeshwa kando ya maduka na barabarani nayo yamesombwa na maji na kuharibiwa.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Marko Ng'umbi, amethibitisha hadi sasa kaya 157 zimeathiriwa na mafuriko hayo.

Kati ya familia hizo, kaya moja yenye watu zaidi ya 10, hawana makazi baada ya nyumba yao kubomoka ukuta wa upande mmoja huku upande mwingine ukiwa na nyufa.

"Hii ni hatari kuendelea kuishi hapa, wameenda kwa ndugu zao eneo la Murombo kuishi kwa muda wakati wakipisha kipindi hiki cha mvua kiishe," alisema Ngumbi anayekaimu nafasi hiyo kwa niaba ya Mkuu wa wilaya hiyo, Emanuela Kaganda.

Pia, alitoa maelekezo kwa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kwenda kuzibua kalavati zote zilizozibwa na uchafu ili kuruhusu maji.

WAATHIRIKA WAFUNGUKA

Mkazi wa Kisongo, Tatu Kisaburi, alisema mafuriko hayo yamesababisha apoteze kila kitu kilichokuwamo kwenye nyumba yao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Ojung'u Salekwa, alisema mvua hiyo ilioanza kunyesha saa 2:30 usiku, Aprili 10.

"Kuna familia moja ya mtoto mchanga, iliokolewa na msamaria mwema, ambaye aliwaokoa mama na mtoto. Hali ya mtoto huyo kwa sasa sio nzuri na wamekimbizwa hospitalini," alisema.

Aidha, alisema sababu nyingine za mafurikio hayo kwenda makazi ya watu ni baadhi ya watu kujenga kwenye njia za maji, na wengine kutupa taka kwenye njia za maji na kuziba mitaro.

Salekwa alisema, watachukua hatua kuanzia sasa za kuwashawishi watu wote waliojenga kwenye njia za maji na makorongo kuondoka kwa hiari.

Diwani wa Kata ya Kisongo, Godson Loning'o, alisema mafuriko hayo yameacha hasara kubwa katika eneo hilo la Kisongo, baada ya kusomba gari la Mwenyekiti wake wa Serikali ya Kijiji.

Nipashe ilipozungumza na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Engorora, Justine Joel, alisema gari lake lenye namba za usajili T.134 DFK, aina ya Toyota IST ilisomba na kukutana nayo kwenye njia panda, akitoka ofisini kwake kurudi nyumbani.

"Tulipovuka eneo la ofisi ya kijiji, ghafla nilikutana na maji mengi, ambayo sijawahi kuyaona eneo hili tangu nizaliwe, ambayo yalisababisha gari langu kuzima," alisema.

Alisema milango iligoma kufunguka, hali iliyowalazimu kutokea kwenye madirisha ya gari na kusombwa na maji, wakiwa wameshikana yeye na abiria wake Godwin Mollel.

Mmoja wa wafanyabiashara waliopoteza bidhaa, Wilson Pelo, alisema alikuwa ameshusha malori mawili yaliyokuwa na shehena ya mifuko ya saruji juzi. "Nalia kwa sababu nimebaki masikini, Shilingi milioni 10 zimeteketea," alisema.

SIMULIZI MAMA ALIYEOKOLEWA NA MTOTO

Lidya Mollel, mkazi wa Kijiji cha Ngorbob, amesema yeye na mwanawe mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu waliokolewa na msamaria mwema baada ya kumpandisha juu ya ukuta na kumrusha mtoto wake juu ya bati, ambako alinyeshewa na mvua hadi ilipokatika.

"Nilikuwa nimelala na mwanangu kitandani, kidogo nikaona maji yameingia ndani, nikaanza kupiga kelele uwii! mtoto wangu, ghafla maji yakajaa kitandani mtoto akaanza kuelea kwenye maji. Nilikuwa nalia nisaidieni mtoto wangu jamani, nakufa na maji na mtoto.

"Saa hiyo maji yalikuwa yamejaa ndani na vitu vyote vimesombwa; nguo na godoro vyote vimetolewa na maji nje."

Siku nne zilizopita, watu wawili wa familia moja wakazi wa Kijiji cha Ilkirevi, Kata ya Olturoto, Wilaya ya Arumeru, walipoteza maisha, baada ya nyumba waliyokuwa wamelala usiku wa manane kuangukiwa na uzio wa jirani yao, baada ya mvua kubwa iliyonyesha kusababisha ardhi kumong'onyoka na kuleta maafa.

Waliopoteza maisha ni baba mzazi wa familia hiyo, Loriv Noah na mwanaye Glory Noah, huku mama wa mtoto huyo (jina lake halijatambuliwa) akinusurika baada ya kuangukiwa na ukuta.

# Timu wataalamu yaanza kusaidia waathirika wa mafuriko ya Rufiji

Na Halfani Chusi

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (pichani) amesema timu ya wataalamu kutoka wizarani zimefika Rufiji, mkoani Pwani kusaidia waathirika wa mafuriko.

Amesema timu hiyo, ikiongozwa na mawaziri, inajumuisha wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Wenye Mahitaji Maalum na Wizara ya Maji.

Jenista alibainisha hayo jana alipofika Rufiji na msafara huo, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa la kuelekeza mawaziri waende wilayani Rufiji kuangalia na kusaidia waathirika hao.

Akizungumza na wakazi wa eneo hilo, Waziri Jenista alisema mafuriko hayo yalitabiriwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) tangu Julai, yakirejewa pia Agosti na Septemba mwaka jana, kwamba nchi tapata mvua ya El-Nino itakayoungana na mvua ya masika na vuli.



Alisema TMA ilitahadharisha kuwa mvua hiyo ingesababisha maafa kwa wananchi kama ilivyotokea wilayani Hanang', mkoani Manyara ambako watu 89 walipoteza maisha.

Alisema walipopewa tahadhari na TMA, Rais aliagiza kuwapo mpango wa dharura kuhakikisha wanaokoa mali na maisha ya watu.

"Nimesikitika pia kwenu (Rufiji) tahadhari ilishatolewa haya ni madhara ambayo tutayapata katika kipindi cha masika, wanachotakiwa kufanya wananchi ni kusikiliza maelekezo ya serikali kazi yetu ni kuhakikisha uhai, uhai, uhai... na huduma za msingi ziendele kupatikana mpaka mapito haya yapite hatutaraji kuona mtu anapoteza maisha wakati tuna uwezo wa kumwokoa.

"Lipo Jeshi la Uokoji hapa, usalama na uhai upo chini ya Waziri wa Mambo ya Ndani, kila mtu kwa nafasi yake anajaribu kuangalia nini afanye, leo tumezunguka na chopa kuona hali ya mafuriko ilivyo, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha uhai wa wananchi.

"Mmesikia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum wataalamu wake wako hapa, tutawapeleka na maeneo mengine nchini, tusingependa kuona kunakuwa na magonjwa ya mlipuko.

"Watalamu wa afya na wataalamu wa ustawi wa jamii nimewaagiza wawatambue na kuwasaidia wenye uhitaji maalum kwa maana ya wajawazito, wajane, watoto, watu wenye ulemavu na wazee, wahakikishe wanagawa dawa za kuzuia magonjwa ya mlipuko pamoja na kupatikana kwa maji safi na salama bila kusahau chakula.

"Leo mmeondoka kwenye nyumba zenu, mmebaki na chakula kidogo cha kuwasaidia kwa siku mbili tatu hizi, baada ya hapo hamwezi kurudi kule mlikotoka, mlikuwa na ndizi, mihogo, ilikuwa kama huna ugali unachemsha ndizi unakula, tuumeshaamua lazima chakula kiletwe cha kutosha, tayari kipo njiani kitaingia leo na kesho," aliahidi

Pia aliwataka viongozi wa wilaya kukigawa chakula kwa waathirika pekee, ikibainika kimegawiwa kinyume, hatua kali za kisheria zitachukuliwa huku akiahidi kufuatilia.

Alisema serikali ilishapeleka mahindi lakini sasa inapeleka unga, maharage na mafuta ya kula ili kuwaondolea adha ya kwenda mashineni kusaga.

Alifafanua kuwa kutokana na shule kuhifadhi baadhi ya waathirika, kutafutwe njia mbadala ya kujenga makazi ya muda kwa kutumia mahema au kufanya kitu kingine chochote.

"Tumekuja hapa tumetimia, kila mmoja aangalie sekta yake, na tukitoka hapa kila ofisi inakwenda kutimiza majukumu yake, tunarudisha taarifa kwa Waziri Mkuu ili aendele kuturatibu.

"Mafuriko yameharibu miundombinu ya umeme, lakini tayari timu ya TANESCO inafanya tathmini na kutatua tatizo hapohapo," alisema.

Mratibu wa Maafa Mkoa wa Pwani, Roseline Kimaro alisema mafuriko hayo yameathiri kata 12 kati ya 13 za Wilaya ya Rufiji.

Alisema mashamba yameathirika zaidi huku akishukuru serikali kupeleka chakula cha msaada na malazi, akisisitiza sasa mambo yameanza kuwa mazuri.

"Serikali imetupatia boti mbili kwa ajili ya kuokoa waathirika waliozungukwa na maji, kuna watoto, wazee, watu wenye ulemavu na wengine mbalimbali hawana uwezo," alisema Roseline.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Muhoro, ambayo ndio imeathiriwa kwa kiwango kikubwa, alisema asilimia 75 ya eneo hilo limekumbwa na mafuriko.

**MVUA ZAIDI**

Wakati huo TMA imetabiri kuwa kuanzia jana hadi kesho kutakuwa na mvua kubwa huku ikiwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa leo mikoa ya Dar es Salam, Tanga, Morogoro, Pwani (visiwa vya Mafia), Lindi, Mtwara, Rukwa, Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma na Visiwa vya Unguja na Pemba inatarajiwa kuwa na mvua kubwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz
NFRA

TANGAZO KWA UMMA

UFAFANUZI KUHUSU UTUMIAJI WA MIKATABA YA MBELE YA UNUNUZI WA MAHINDI NA MPUNGA NA KUANZA KUTUMIA MIZANI ZA KIDIGITALI WAKATI WA UNUNUZI WA NAFAKA

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula Nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, NFRA hununua nafaka kwa ajili ya Akiba ya Taifa ya chakula. NFRA inatarajia kununua Mahindi Meupe na Mpunga katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2024/2025, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024. Ununuzi utafanyika kupitia kanda nane za Wakala ambazo ni Arusha, Dodoma, Kipawa (Dar es Salaam), Makambako, Songwe, Shinyanga, Songea na Sumbawanga.

Kipindi cha **tarehe 26 Machi, 2024** hadi **tarehe 03 Aprili, 2024,** NFRA ilitoa Matangazo ya kununua mahindi na mpunga kwa utaratibu wa mikataba ya mbele kutoka kwa **Wakulima na Wafanyabiashara wakubwa.** Sambamba na Tangazo hilo, NFRA inaujulisha Umma kwamba utaratibu wa kununua nafaka kupitia vituo vya ununuzi katika maeneo mbalimbali Nchini unaendelea kutumika wakati wa msimu wa ununuzi wa nafaka. Utaratibu huu unawezesha **Wakulima wote wadogo** kuweza kuuza nafaka zao moja kwa moja kwa NFRA bila kuwa na mikataba. Msimu wa 2023/2024 NFRA ilifungua vituo vya ununuzi sabini na saba (77) na inatarajia kufungua vituo zaidi vya ununuzi kwa msimu wa 2024/2025 katika maeneo mbalimbali Nchini.

Aidha, ili kuongeza uwazi katika vipimo wakati wa utekelezaji wa zoezi la ununuzi wa nafaka, NFRA inaujulisha Umma kwamba kuanzia msimu ujao wa ununuzi wa nafaka (2024/2025), itatumia mizani za kidigitali (digital weighing scales) kupima uzito wakati wa kununua nafaka kutoka kwa Wakulima. Vituo vyote vitakavyofunguliwa vitatumia mizani hiyo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi ya ununuzi wa nafaka na kupunguza malalamiko wakati wa upimaji wa nafaka zinazoletwa kuuzwa kupitia vituo vya NFRA.

Baada ya ufafanuzi wa hapo juu, Wakulima wote mnakaribishwa kuuza nafaka NFRA msimu wa ununuzi utakapoanza.

**Imetolewa na:**

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,**
**Tarehe 08 Aprili, 2024.**
**Simu Namba: +255 (0) 26 2963953**
**Baruapepe: info@nfra.go.tz**



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainabu Abdallah (katikati), akipanda mche wa mti kuzindua kampeni ya upandaji miti wilayani humo, ijulikanayo kama "Soma na Mti" katika Shule za Sekondari za Kata ya Potwe na Kwabastola Kata ya Makole juzi, ambapo miti takribani 4000 ilipandwa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Aliyetumbuliwa kisa corona arejeshwa kazini

**Na Romana Mallya**

IKIWA ni miaka mitatu na miezi 11 tangu aliyekuwa Mkurugenzi wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (NPHL) Dk. Nyambura Moremi, kuondolewa katika nafasi hiyo ili kupisha uchunguzi baada ya kubainika kasoro za ya kiutendaji, amerejeshwa katika nafasi hiyo.

Jana, katika mitandao ya kijamii, kulikuwa na taarifa ya salamu za pongezi kwa Dk. Moremi kutoka NPHL iliyo chini ya Wizara ya Afya, kumpongeza kwa kuteuliwa kuwa mkurugenzi wa taasisi hiyo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Afya, Englibert Kayombo, alithibitisha kuhusu taarifa ya kurejeshwa kwa Dk. Nyambura katika nafasi ambayo alikuwa akiitumikia awali.

Mei 3, 2020 aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, wakati akimwapisha Waziri wa Katiba na Sheria, alibainisha changamoto za utendaji wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii na aliyekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alichukua hatua.

Siku hiyo hiyo, Waziri Ummy kupitia taarifa yake kwa vyombo vya Habari, alimwelekeza aliyekuwa Katibu Mkuu (Afya) kuwasimamisha kazi mara moja Dk. Moremi na Jacob Lusekelo, Meneja Udhibiti wa Ubora ili kupisha uchunguzi.

Kadhalika, aliunda kamati ya wataalam wabobezi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mwenendo wa NPHL ikiwamo mfumo mzima wa ukusanyaji na upimaji wa sampuli za UVIKO-19.

Kamati ilipewa kazi hiyo na kutakiwa kuikamilisha Mei 13, 2020 ili kuwasilisha taarifa kwa waziri husika.

Magufuli alionyesha shaka kuhusu ufanisi wa maabara hiyo baada ya kupima sampuli za matunda na wanyama na baadhi kukutwa na maambukizi ya UVIKO-19.

Mei 23, 2020 serikali katika ripoti ya uchunguzi, ilibaini kasoro mbalimbali za kiutendaji zilizokuwamo katika maabara hiyo.

Waziri Ummy akiwasilisha siku hiyo taarifa ya ripoti hiyo, alitaja upungufu uliobainishwa na kamati hiyo kuwa ni Pamoja na moja kati ya mashine za kupima sampuli za UVIKO-19 ilikuwa na hitilafu bila uongozi wa maabara kuchukua hatua za kuifanyia matengenezo.

Taarifa hiyo pia ilibaini kuwapo kwa upungufu katika mfumo wa kimuundo, kiutendaji na uendeshaji wa kitaaluma katika upimaji wa vipimo, uhakiki wa ubora wa majibu na udhaifu katika uhifadhi wa vipimo vya UVIKO-19.

Waziri Ummy alisema kamati hiyo pia, imetaja kuwapo kwa upungufu wa wataalamu wenye sifa za mafunzo ya "Biotechnology and Molecular Biology" katika sekta ya afya ikiwamo katika maabara hiyo.

Pia kutokana na taarifa ya kamati kuhusu upimaji wa sampuli za ugonjwa wa UVIKO-19, wizara ilichukua hatua ya kuhamisha shughuli za upimaji wa UVIKO-19 kutoka kwenye maabara iliyoko Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Dar es Salaam na kuanza kutumika kwa mashine zingine za maabara mpya iliyoko Mabibo, Dar es Salaam.


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MBEYA

RUFAA YA MADAI NA 10/2023

(Kutoka shauri la Marejeo Na 1/2023 kutoka Mahakama ya Wilaya Songwe,asilia shauri la maombi ya madai na 21/2021 ya Mahakama ya Mwanzo Mwambani mbele ya Mh.E.E.Mtengeti)

ZAKAYO MATIGA..................MRUFANI

DHIDI YA

SAID MOHAMED SOOD, FAGIO COURT BROKER, GASTORY MARANDU.....WAJIBU RUFAA

KWA BWANA: GASTORY MARANDU

POPOTE ULIPO-TANZANIA
KUITWA SHAURINI

Unaamuliwa na Mahakama hii,kuhudhuri hapa Mahakamani siku ya tarehe 09/05/2024 siku ya Jumanne saa 3:00 asubuhi bila kukosa. ELEWA KWAMBA, ukikosa kufika siku hiyo,shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 04/04/2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA



## TANGAZO LA MNADA

Held, Marmboto ,shashinshale na **Crisam Auctioneer** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari na kiwanja Jijini Dar es salaam na Arusha Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada

| Jina la mdaiwa | DHAMANA | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Baraka Nyang'anyi Marela | Toyota Passo T698 DWD | 26.04.2024 |
| Robert Job Mtyani | Toyota Verossa T641 CEF | 26.04.2024 |
| Daniely Yolimi Ngajilo | Subaru Forester T348 EDZ | 26.04.2024 |
| Mohamed Mahmoud Osman | Toyota Passo T822DCJ Ipo Dar es salaam | 26.04.2024 |
| Salvatory Matei Mwacha | Kiwanja kipo Mkonoo Arusha | 26.04.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

Kwa Mawasiliano Piga 0677014355(Fanikiwa)


# Bomoabomoa Msimbazi kuanza rasmi

**Na Romana Mallya**

UBOMOAJI wa nyumba 2155 zilizoko katika Bonde la Msimbazi, jijini Dar es Salaam, unatarajia kuanza leo kama ilivyotangazwa awali. Bomoabomoa hiyo inafanyika baada ya fidia ya Sh. bilioni 52.61 kwa ajili ya kupisha mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kutolewa kwa wakazi wa eneo hilo.

Akizungumza hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Miradi ya Ushirikiano na Benki ya Dunia na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Humphrey Kanyenye, alisema watu 2,155 kati ya 2,329 walioko kwenye daftari la kwanza wamekwishapokea malipo yao.

Alibainisha kuwa kituo cha mabasi ya mwendokasi (yard) kitahamishiwa Ubungo Maziwa na pia wanatarajia kujenga City Park itakayoongoza kwa ukubwa mkoani Dar es Salaam.

Kanyenye alisema lengo la kujenga mto huo ni kuzuia mafuriko yanayotokea katika eneo hilo. Alisema ofisi ya uratibu wa mradi kwa kushirikiana na ofisi za wakurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni zimeshatoa taarifa kuanza ubomoaji wa nyumba zilizofidiwa kuanzia leo. Mradi huo unahusisha ujenzi wa daraja, ujenzi wa mto na kuhamisha kituo cha mabasi ya mwendo kasi na kujenga City Park. Mradi huo utagharimu Dola za Kimarekani milioni 260.

# Wafanyabiashara soko la madini walilia vibali

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA katika soko kuu la madini mkoani Arusha, wameiomba serikali kuwapatia kibali cha kuanza kuuza Tanzanite kama ilivyoahidi badala ya kuendelea kukaa kimya, hivyo kuendelea kufanya biashara katika mazingira magumu.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kati wa Madini, Jeremia Kituyo, alisema wanakabiliwa changamoto mbalimbali ikiwamo kuzuiwa kuuza Tanzanite na leseni kuwa na mipaka na kushindwa kununua bidhaa hiyo katika maeneo mengine.

Alisema serikali iliwaahidi ifikapo Machi, mwaka huu, wataanza kuuza madini hayo lakini mpaka sasa imekuwa kimya na hakuna taarifa waliyopatiwa kuhusu kinachoendelea au ni jambo gani limekwamisha wasianze kuuza kama walivyoahidiwa.

Kituyo alisema madini ya Tanzanite yamekuwa ya eneo moja na wengine hawaruhusiwi kuuza na hiyo imekuwa changamoto kubwa na kusababisha wafanyabiashara wa madini mkoani Arusha kuishi katika mazingira magumu.

"Zaidi ya miaka mitatu ilizuiwa. Biashara ya Tanzanite imeleta changamoto na hali zetu ni mbaya. Tuna vijana 30 ambao walifundishwa ukataji wa madini wameshindwa kuendelea na hii biashara na mashine zao zimefungiwa ndani. Tunaishi mazingira magumu na Tanzanite ndio inatufanya tuuze na mawe mengine.

"Huyu Mkuu wa Mkoa, Paul Makonda, tuna imani atatusaidia kurejesha soko la Tanzanite. Tuliambiwa tutaanza kuuza Tanzanite lakini mpaka sasa ni changamoto na tatizo lingine ni suala la leseni. Haturuhusiwi kutumia katika mikoa mingine mwisho wake ni hapa Arusha. Nikitaka kwenda mkoa wa Geita kununua madini natakiwa nikate leseni nyingine hili jambo linatutesa, "alisema Kituyo.

Kituyo alisema leseni wanayoilipia Sh. 250,000 wamepewa masharti magumu kwa kuzuiwa kwenda kununua madini mikoa mingine jambo ambalo serikali inatakiwa kuliangalia ili wasiendelee kufanya kazi zao katika mazingira magumu.

Method Shayo alisema soko hilo ni kubwa na kuna uwezekano wa kuishia pabaya licha ya kutegemewa Afrika Mashariki kwa kuwa wana mawe kutoka nje ya nchi na matokeo yake wafanyabiashara wa kati wa madini wameminywa.

"Kuondolewa Tanzanite katika hili soko kumesababisha uzorotaji mkubwa kwa sababu madini mengine hayauziki. Jambo lingine hatuna uhuru na haya madini yamegeuzwa kama dawa za kulevya. Hili jiwe nikitoka nalo nje ya soko hata kama nina leseni ninaitwa mtoroshaji, sina uhuru na hii biashara yangu," alisema Shayo.

Naye Joyce Masanja alisema changamoto nyingine ni watu wanawachukua wageni walitoka nje ya nchi na kupelekwa moja kwa moja katika machimbo ya madini na wazawa kushindwa kunufaika na madini.

"Mgeni anatoka Ulaya anaenda moja kwa moja kwenye machimbo. Anaenda kufanya biashara pembeni ya machimbo sasa sisi tutakula wapi? Huyo mgeni hana ofisi anauza zake anaondoka. Tunachotaka ni wote turuhusiwe kuuza tanzanite hapa Arusha ukiitafuta tanzanite huipati na watalii wanaipenda," alisema Masanja.

Mfanyabiashara mwingine, Tumaini Laizer, alisema wafanyabiashara wa tanzanite wengi wao wamefilisika wameenda kwenye kilimo baada ya kuzuiwa soko hilo kuuza madini hayo.

Alisema tatizo jingine ukubwa wa soko hilo haliendana na uhalisi kwa kuwa mazingira yake hayawavutii, hivyo inahitajika uboreshaji unaoendana na thamani ya bidhaa wanayoifanya.

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| | | 2023 | 2022 |
|---|---|---|---|
| A | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 12,803 | 13,063 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 17,855 | 11,080 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 37,576 | 39,601 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,667 | 1,287 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (4) | (69) |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 27 | 27 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 106,652 | 96,560 |
| 12 | Mali Nyingine | 12,269 | 11,892 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 14,712 | 13,865 |
| | **JUMLA YA MALI** | **205,595** | **187,346** |
| B | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 10,790 | 2,038 |
| 18 | Amana za Wateja | 139,395 | 125,950 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 448 | 8 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 1 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,290 | 2,787 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 8,044 | 8,044 |
| 27 | Dhima Nyingine | 9,784 | 9,674 |
| 28 | Madeni | 8,350 | 17,000 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **180,102** | **165,502** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **25,493** | **21,844** |
| C | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 27,797 | 27,797 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (19,215) | (15,276) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 0 | 0 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 16,910 | 9,322 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,493** | **21,844** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,111 | 1,335 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 8,131 | 8,239 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,869 | 5,360 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 60 | 75 |
| D | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.4% | 11.7% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.4% | 8.1% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 71.7% | 78.9% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 51.9% | 54.5% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70.2% | 72.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 17.8% | 3.8% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 9.7% | 4.7% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | 2023 | 2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 28,403 | 25,393 |
| 2 | Gharama za Riba | (8,232) | (6,870) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 20,171 | 18,523 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 1,213 | (4,394) |
| 6 | Mapato Yasiyo ya Riba: | 5,346 | 5,655 |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 500 | 384 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 4,747 | 4,818 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 98 | 452 |
| 7 | Gharama Zisizo za Riba: | (28,270) | (24,790) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (15,617) | (14,164) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (12,654) | (10,627) |
| 8 | Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | (1,540) | (5,007) |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (473) | (2,023) |
| 10 | Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | (2,013) | (7,030) |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 1 |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | (2,013) | (7,029) |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 335 | 384 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (72) | (253) |
| 15 | Idadi ya Matawi | 17 | 18 |
| | BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.0% | -3.8% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -7.9% | -32.2% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 111.0% | 99.0% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 14.1% | 13.5% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (2,013) | (7,030) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| - Hasara Katika Mali | 715 | 7,194 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,965) | (18,851) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (139) | (0) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 22,637 | 5,201 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 5,393 | 8,535 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 760 | 335 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (11,466) | 10,942 |
| - Kodi Iliyolipwa | 473 | 203 |
| - Mengineyo (bainisha) | 0 | 1,476 |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | 8,394 | 8,004 |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,659) | (822) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 165 | 0 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (2,947) | (7,471) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (5,442) | (8,292) |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 5,663 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (940) | (841) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | 4,723 | (841) |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 7,675 | (1,129) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 19,266 | 20,395 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 26,942 | 19,266 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2023

| | Mtaji wa Hisa | Hisa za Upendeleo | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2023 | 27,797 | 5,960 | 2,432 | (15,276) | 930 | 0 | 21,844 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | (2,013) | 0 | 0 | (2,013) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 5,663 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5,663 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 0 | (1,926) | 1,926 | 0 | 0 |
| Mengineyo (Tangulizi la mtaji wa Hisa) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2023 | 27,797 | 11,623 | 2,432 | (19,215) | 2,856 | 0 | 25,493 |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022 | 27,797 | 0 | 2,432 | (12,101) | 4,857 | 5,888 | 28,874 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | (7,030) | 0 | 0 | (7,030) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 5,960 | 0 | (72) | 0 | (5,888) | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 0 | 3,927 | (3,927) | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2022 | 27,797 | 5,960 | 2,432 | (15,276) | 930 | 0 | 21,844 |

## BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAYOISHIA 31.12.2023

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezi-tathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Mwenyekiti Catherine Kimaryo | ______ | ______ |
| 2. Mkurugenzi Prof. Josephat Lotto | ______ | ______ |




MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaokwepa kodi katu wasionewe huruma, wanakwamisha maendeleo

**RAIS** wa kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema suala la kulipa kodi ni la msingi kwa taifa lolote na kama jambo hilo halifanyiki, maendeleo yatakuwa ndoto kupatikana. Pia alisema taifa lolote ambalo wananchi wake hawalipi kodi, rushwa huchukua nafasi yake.

Msemo huo wa Nyerere licha ya kwamba miaka mingi imepita, bado una mashiko ndiyo maana mataifa yote duniani, Tanzania ikiwamo, yanahimiza suala ulipaji wa kodi na ndicho chanzo kikuu cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mantiki hiyo, taifa linapokusanya kodi kwa wingi ndivyo kasi ya maendeleo inavyokuwapo.

Kutokana na umuhimu huo, Serikali ya Tanzania na ile ya Mapunduzi Zanzibar (SMZ) zilianzisha taasisi kwa ajili ya usimamizi wa ukusanyaji kodi na mapato yatokanayo na kodi kama vile za ushuru wa forodha, mafunzo ya ufundi na ongezeko la thamani (VAT) zimekuwa zikitangazwa kuongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa sasa, makusanyo hayo yamepanda kutoka Sh. trilioni 18 mwaka 2021/22 hadi Sh. trilioni 24 mwaka 2022/23.

Makusanyo ya mapato hayo pamoja na yale yasiyo ya kodi, yanayokusanywa katika mamlaka za serikali za mitaa, yamesaidia kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya serikali kama vile barabara, maji, umeme vijijini, elimu na afya. Kadri makusanyo yanavyoongezeka ndivyo kasi ya miradi ya maendeleo pia inavyokuwa. Aidha, bila kodi hakuna maendeleo endelevu.

Pamoja na jitihada hizo za serikali kusisitiza umuhimu wa kulipa kodi ili kuleta maendeleo endelevu kwa nchi, bado kuna ukwepaji unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kwa kushirikiana na maofisa wa serikali wakiwamo wale waliopewa jukumu la kutekeleza wajibu huo.

Akizungumza juzi wakati wa Baraza la Eid el Fitr jijini Dar es Salaam, Rais Samia Suluhu Hassan alisema kuna mtandao wa wafanyabiashara, viongozi wa siasa na maofisa wa serikali wa ukwepaji wa kodi ambao unakwamisha juhudi za serikali katika kufikia malengo ya makusanyo ya mapato na hatimaye kukwamisha shughuli za maendeleo.

Rais alisema licha ya ukwepaji kodi kuna wafanyabiashara, watumishi wa serikali wakiwamo waumini wa dini ambao wanachezea mifumo ya kodi kwa lengo la kujinufaisha, hivyo kuwasihi viongozi wa dini kusaidia katika udhibiti wa tatizo hilo. Sambamba na hilo Rais alisisitiza kuwa hata alipomwapisha Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alimsisitiza akusanye kodi na zile za dhuluma aache bali atende haki anapotekeleza wajibu huo.

Ni dhahiri kwamba kodi ni msingi mkuu kwa maendeleo ya taifa lolote na kama suala hilo halitasimamiwa ipasavyo, kuna hatari ya kuporomoka kwa uchumi kunakoendana na kukithiri kwa vitendo vya rushwa. Ukwepaji kodi una madhara makubwa lakini pia matumizi ya nguvu katika ukusanyaji wa mapato hayo ya serikali ni chanzo cha kuwapo kwa tatizo hilo.

Ukwepaji kodi au kuchezea mifumo ya kodi ni moja ya vitendo vinavyohesabika kuwa ni uhujumu uchumi kwa sababu mtu anapofanya hivyo, ama kuingiza bidhaa kwa njia ya magendo au kushirikiana na maofisa wa serikali kufanya udanganyifu wa aina yoyote, haikubaliki hata kidogo.

Kama alivyoagiza Rais Samia, ni vyema viongozi wa dini wakalisisitiza jambo hilo kwa sababu madhara yake ni makubwa kwa taifa. Viongozi wa dini wanapaswa kukemea vitendo hivyo kama wanavyofanya katika masuala ya ufisadi, rushwa, katiba mpya, ukatili na ndoa za jinsia moja.

Kutokana na umuhimu wa kodi kwa maendeleo, wale wote wanaobainika kukwepa kodi wachukuliwe hatua kali za kisheria na ikiwezekana sheria zibadilishwe ili kuwabana zaidi na kuwaadhibu watu wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Huwa nadumu na imani, kinamama tukiondolewa mzigo huu, tunaweza!

**JAMII** ilikofika sasa, inapaswa kutambua kuwa mwanamke ana mhimili mkubwa unaowezesha gurudumu la maisha.

Wanawake wanapoamua pamoja, daima wanaweza. Hivyo, kinamama wanapaswa kuongoza watoto wa kike wenzao, waweze kutambua nafasi yao na kujua kilicho sahihi na kinachofaa katika maisha na kipi hakistahili kuwa nacho.

Hivyo, wanaweza kufahamu mambo mbalimbali, ikiwamo anayopitia mwanamke katika umma unaomzunguka, hivyo watu wote kwa ujumla wanapaswa wakumbuke nafasi ya mwanamke ilivyo katika jamii.

Ndani ya jamii za Kiafrika, zimekuwa na mtazamo tofauti kwa kinamama, kwa wanachokiamini kuwa mwanamke ni mfanyakazi za nyumbani na hana kitu kingine cha kufanya.

Hiyo, inawafanya baadhi ya kinababa wengi kutumia fursa hiyo kuwatumikisha wanawake bila ya huruma. Wanawake hawaruhusiwi kuwa na kauli sehemu yoyote.

Mwanamke anashinda nyumbani, akitekeleza majukumu yote na katika baadhi ya maeneo vijijini tunasikia huko, Tarime na Songea na vingine vingi hivyo wanaume walio wengi wana watumikisha wake zao bila kujali kama wamechoka au vinginevyo.

Majukumu yaliyozoeleka, yanajumuisha kukata kuni za mapishi, kuchota maji, hata wanaume ninawasihi peaneni elimu katika kuamini mwanamke, ana haki kwani hata yeye anachoka hivyo anatakiwa kupumzika.

Hata hivyo, bado watu walio wengi nadhani elimu hiyo haijazama kwao kisawasawa, kuna baadhi ya makabila yanayopenda kurithi wanawake, mila mbaya na iliyopitwa na wakati.

Ni jambo baya na si sahihi kumrithi mwanamke, kwani ni unyanyasaji uliopitiliza na ni makosa makubwa kisheria.

Ni dhahiri katika hilo, anayehusika na tendo hilo anabaki kuwa mgandamizaji wa haki na uhuru wa kijinsia kwa mwanamke husika, jambo ambalo sio la kiungwana na linakemewa vikali

Hivyo, mwanaume anayefanya jambo hilo la kumrithi mjane, anapaswa kuchukua hatua, kwani sio vyema. Naye, mwanamke anayo nafasi kubwa katika jamii kwani, kinamama tunao uhuru wa kushiriki kwenye kampeni ikiwa tunaelekea mwaka wa uchaguzi huu 2024 na wa uchaguzi mkuu 2025.

Inatupasa na kukumbuka kwamba, tuna nafasi ya kuwa wazalendo katika kushiriki kwenye uchaguzi kikamilifu, kukiwapo maono ya kuwania cheo. Kwa chochote kile, ni vyema mtu akajitambua anakoelekea.

Wewe mama nakushauri, chukua fomu za kuwania nafasi bila ya kuchelewa, hali itakayosaidia ushindani wa hali ya juu na kuwafanya wanawake kung'ara juu wakishika nyazifa za kuamua katika madaraka ya nchi.

Hivyo, nawasihi wenzangu, msiache kuwa na malengo ya kutimiza ndoto zenu, kwani kuna baadhi ya wazazi hasa vijijini, wamekuwa na mtazamo tofauti katika malezi ya watoto wengi wao, wakiamini kuwa mtoto wa kike hawezi jambo lolote la kufanya. Jambo hilo si la kweli hata kidogo tena!

Kuna falsafa kwamba, mwanaume ndiye mwenye haki ya kurithi na mengine mengi ya aina hiyo, jambo ambalo sio la kweli. Mimi naamini uhalisia, binti ana nafasi kubwa kuikomboa jamii hiyo inayomhusu. Mama huwa ana uthubutu, pale jamii ikimpa haki na uthubutu wa kujikomboa kuanzia na elimu.

Ni chanzo cha maendeleo na inatupasa kukumbuka kuna vyombo vinavyotetea haki za wanawake.

Wanawake wana fursa mbalimbali za maendeleo, kwani hata Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), kimeonyesha mfano kwa kutambulisha mradi mpya wanawake mnamo Oktoba, 2020.

Inatambua kuwa ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi, hasa ya kisiasa, bado ni mdogo, hivyo ina azma ya kuwakwamua kushiriki kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Bila shaka, hata watoto wa kike walioko shuleni wasome kwa bidii, kwani wanayo nafasi ya kuongoza inahitaji elimu, hata kuwawezesha kuvuka katika malengo yao.

Niseme, bila ya kusahau napo wapo kinababa wanapaswa kupeana elimu ya utambuzi wa nafasi ya mtoto wa kike na kina mama kwa ujumla, taifa letu lizidi kuwa imara zaidi.

TANGAZO

# FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

1st Housing
Homes within your reach

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2023

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2023 | Mwaka uliopita 31st Dec. 2022 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 149 | 1,532 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,600,562 | 3,601,363 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,986,264 | 6,695,407 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 27,439,967 | 19,561,504 |
| 12 | Mali Nyingine | 843,009 | 706,753 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 230,990 | 323,876 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **37,722,941** | **32,512,435** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,880,605 | 911,787 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 557,439 | 793,444 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 41,070 | 41,070 |
Mashauri ambaye pia ni Mwezeshaji wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Mkoa wa Mara akizungumza katika semina ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari 20 kutoka mkoani hapa, alisema uwekezaji kwa mtoto unatakiwa kuanza akiwa bado mdogo ili kupata kizazi chenye uwezo kiakili na maadili.


Alisema ili kuwa na kizazi kilicho bora, serikali kupitia halmashauri inapaswa kutenga bajeti hiyo itakayowagusa watoto na kuwataka waandishi kuandika habari zinazohusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kupitia mradi wa mtoto kwanza ili kutoa elimu kwa jamii.

"AICT Dayosisi ya Mara na Ukerewe kupitia mradi wa mtoto kwanza unaratibu programu Jumuishi ya Taifa wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT -MMMAM) inalenga kutoa huduma za afya, lishe, malezi yenye mwitikio, ujifunzaji wa awali na ulinzi na usalama kwa watoto wa miaka sifuri mpaka nane," alisema Mashauri.

Alisema katika kuimarisha Ushirikiano wa Wadau wa sekta mbalimbali katika Huduma za MMMAM, programu hiyo inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26.

Vilevile, alisema mradi wa Mtoto Kwanza unatekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu ukifadhiliwa na Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali Tanzania (TECDEN) kuanzia 2022 hadi 2024.


Baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki katika semina hiyo, akiwamo Frankius Chilophas, alisema kuna haja jamii kuwekeza kwa mtoto wakati wa kukua ili kumuimarisha kiafya, kiakili na kimaadili na kuwa na kizaji chenye tija.




Hili la kulipana posho tofauti linafikirisha




BUFE
IJUMAA APRILI 12, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



MIAKA 40 BILA YA SOKOINE

**Ujue Upekee wake Edward Sokoine, hata akapewa siku ya kukumbukwa**

# Miaka 40 bila ya Sokoine

**Na Sabato Kasika**

LEO inatimu miaka 40 tangu kufariki aliyekuwa Waziri Mkuu katika serikali ya awamu ya kwanza, Edward Moringe Sokoine, mwaka 1984.

Hapo anakumbukwa kwa mengi, hasa alivyopigania maendeleo ya taifa, kwa kujitolea kukabili wahujumu uchumi, akianza na vigogo nchini, ili nchi isonge mbele kimaendeleo.

Akiwa katika nafasi hiyo ya uwaziri mkuu, Sokoine hakuona haya kuwaambia viongozi wa serikali na wananchi, hasa wafanyabiashara, waliokuwa na mali nyingi kuelezea kwa uwazi jinsi walivyozipata.

Katika mazingira hayo, waliojipatia mali isivyo halali walimuona kikwazo, wengi wakimuogopa na wakalazimika kutupa mali zikiwamo fedha, walizopata kwa njia isiyo sahihi.

Kwa ujumla ni kwamba, Sokoine amedumu akiwa kiongozi asiyesita kutoa maamuzi magumu kwa kila aliyeenda kinyume, pasipo kujali kwamba ni kiongozi wa serikali, mfanyabiashara au mtu wa kawaida.

Hivyo, kwa mtindo huo wa uongozi wake wa kutowaonea haya wahujumu uchumi, alipendwa na wanyonge na kuchukiwa na waliojilimbikizia mali walizopata isivyo halali.

Sokoine huyo, sasa ni miongoni mwa viongozi wa kutolewa mfano kwa utendaji bora, kwani alifanya kazi bila ya kuchoka usiku na mchana, pia akichukia rushwa na kutamani nchi ipige hatua kimaendeleo, kiuchumi na kijamii.

Enzi ya uhai wake, aliwahi kukaririwa wakati akihutubia kikao cha Halmashaurin Kuu



Edward Sokoine, katika zama alizotumikia uwaziri mkuu, akipokea mmoja wa wageni kiserikali nchini. **PICHA: MAKTABA**

ya Taifa ya CCM (NEC) mjini Dodoma akitahadharisha kwa kauli kwamba:

"Ole wao wale wanaotumia nafasi zao za umma na serikali, kuiba, kuhujumu uchumi, kupokea rushwa, maana salama yao ni kudra za Mwenyezi Mungu labda nisiwajue!"

Ni wakati aliokuwa akipambana na uzembe kazini, rushwa, ulanguzi na biashara ya magendo, ambazo kila kona ya nchi, walengwa walikuwa na matumbo joto.

Kauli hiyo ikaonyesha wazi ni kiasi gani amepigania kimaendeleo nchini, akiweka pembeni maslahi binafsi. Huyo ndiye Edward Moringe Sokoine, nyota iliyozimika ghafla ikipambania maslahi ya taifa.

**VITA UHUJUMU UCHUMI**

Wakati huo Sokoine, alipoanzisha vita ya uhujumu uchumi, wakati huo kukiwapo uhaba mkubwa wa bidhaa za viwandani, hata ikasababisha wananchi kutafuta njia mbadala za kukabiliana na hali hiyo.

Mojawapo ya njia hizo, inatajwa ni wafanyabiashara kuingiza bidhaa kinyemela au kwa magendo kutoka nchi jirani walikokuwa wakiziuza kwa bei ya juu na kusababisha wananchi washindwe kumudu bei.

Pia, kulikuwapo uzalishaji mdogo viwandani na uhaba wa bidhaa. Serikali ilikuwa ikipanga na kudhibiti bei ya bidhaa, katika mazingira hayo, wafanyabiashara waliamua kuficha bidhaa ili kulazimisha bei kupanda, ili wapate faida mara mbili.

Vikwazo hivyo ndivyo vilivyosababisha serikali ya awamu ya kwanza, kubuni njia ya kuwanasa wahujumu ambayo Sokoine alikuwa akiendelea nayo tangu mwaka 1983 hadi Aprili 12 mwaka 1984 alipofariki dunia.

Kimsingi, vita dhidi ya wahujumu uchumi vilivyoanza awali, vilitikisa kila kona nchini na kusababisha wahusika kutupa mali walizopata isivyo halali sehemu mbalimbali ikiwamo barabarani, mtoni na hata ziwani.

**ALICHOAMINI SOKOINE**

Mara zote, Sokoine kazini akaamini katika haki, usawa, uwajibikaji, siasa ya ujamaa, pia akibeba imani maendeleo yanaweza kupatikana, kutokana na watu kujituma kufanya kazi halali, tena kwa bidii.

Kiongozi huyo, akawasilisha imani katika mabadiliko chanya akianika mtazamo na msimamo wake kwamba: Yu mzalendo kwa taifa lake; mchukia rushwa, uhujumu uchumi, ulanguzi na magendo.

Vilevile kunarejewa mtazamo mwingine wa Sokoine, akadumu katika nadharia kwamba, yu mtu wa vitendo zaidi, akiwa mbali na matamshi ya kupenda kulalamika, yu muumini wa dhana 'hapa kazi tu' na 'kazi iendelee.'

Katika staili yake ya utendaji, marehemu Sokoine anakumbukwa mbali na uzalendo wake wa vitendo, akasonga katika Imani 'siasa ni kilimo' na 'kilimo ni uti wa mgongo wa taifa.'

Katika imani hiyo kwenye kilimo, akitokea bungeni Zanzibar, akaamua kutumia usafiri wa gari badala ya ndege akidhamiria kukagua juhudi za wananchi na mendeleo yao katika kilimo.

INAENDELEA UK.12

# Ujue Upekee wake Edward Sokoine, hata akapewa siku ya kukumbukwa



Gari alilopata ajali nalo hadi kifo, Edward Sokoine, mkoani Morogoro.



Edward Sokoine, alipokuwa akiteta jambo na Rais Julius Nyerere. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Hulka na nafsi yake;**

1. Amekuwa muumini wa Haki, Usawa na Uwajibikaji.
2. Ameamini katika itikadi na siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.
3. Kiitikadi akazama katika msimamo kwamba, maendeleo huja kwa watu kujituma kufanya kazi halali na bidii.
4. Pia, aliamini katika mabadiliko chanya kwa jamii yake.
5. Mara zote akawa mzalendo hasa kwa taifa alilotumikia maisha yake yote.
6. Amechukia vitendo vya rushwa, hujuma, uhujumu uchumi, ulanguzi na magendo.
7. Alikuwa mtu wa vitendo na kamwe alikuwa si mtu wa kupenda kulalamika lalamika.

**Mchango wake kitaifa;**

1. Siku zote akawa mstari wa mbele enzi za vita ya Kagera kupambana na Nduli Idd Amini Dada, aliyetangaza kuteka sehemu ya mkoa wa Ziwa Magharibi, iwe sehemu ya taifa la Uganda.
2. Alianzisha vita dhidi ya Uhujumu Uchumi nchini, biashara ya ulanguzi, magendo na aliichukia rushwa kwa vitendo
3. Mara zote akabaki mzalendo wa kweli wa taifa hili.
4. Amedumu akisimama katika msimamo 'siasa ni kilimo', akiamini 'kilimo ni uti wa mgongo wa taifa', hata kifo chake kilitokea katika hatua ya kuacha kusafiri kwa ndege, ili impe fursa kushuhudia kinachoendelea mashambani na ustawi wake, kutoka juhudi za Watanzania walioko katika sekta hiyo kuu.
5. Alitunza na kutukuza utamaduni wa Kiafrika na utaifa wa Mtanzania.


**SAFARI YAKE KISIASA**

Mnamo Januari 1,1961, akiwa kamaliza elimu ya sekondari, Edward Moringe Sokoine alijiunga na chama cha Tanganyika African National Union (TANU), ikiwa ni miezi michache kabla Tanganyika haijapata Uhuru.

Akiwa mwanachama hai wa TANU, mwaka 1962, alienda Ujerumani Magharibi (sasa zimeungana), ikiwa rafiki wa taifa jipya la Tanganyika, Sokoine akaenda kusomea fani ya Utawala na aliporejea mwaka 1963, alipangiwa kazi Ofisa Mtendaji wa Wilaya (DEO), wilayani Masai, hata akafana kikazi ambako kulikuwa kwao.

Mnamo Septemba 30, 1965, akiwa kijana mdogo wa miaka 27, aliyeonyesha akili na ubunifu mkubwa, akagombea ubunge jimbo la Masai na kumshinda kwa kishindo mpinzani wake, Edward Carli Boniface Ole Mbarnote, aliyekuwa Chifu wa Wamasai. Sokoine alitwaa kura 6,977, Chifu Mbarnote akiambulia kura 871.

Akiwa bungeni, nako akaonyesha umahiri wa uwakilishi wake, kwa umahiri na stadi za uwakilishi, ikiwamo kudai sababu za Wamasai wa Ngorongoro kuzuiwa kulima, wakati hawana mifugo inayowalisha.



Hayati Edward Sokoine.

Ni sehemu ya maono yaliyomfanya kuaminika maradufu mbele ya Rais Julius Nyerere, aliyevutiwa naye, japo katika umri mdogo.

Katika hali iliyoonyesha kuaminika mwaka 1967, Mwalimu Nyerere akamteua kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Mawasiliano, Usafirishaji na Kazi n Mwaka 1970, akamteua kuwa Waziri wa Nchi, huku mwaka 1972, Rais Nyerere akamteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Hata katika ulingo wa kisiasa, heshima na chati yake ilipanda maradufu, pale vyama TANU na Afro Shiraz Party (ASP) kuungana na kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Februari 5, 1977, Sokoine akateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, ambacho ni cheo chenye hadhi nyeti katika siasa ya nchi tangu zama hizo, akidumu nacho hadi kifo chake, siku kama ya leo, mwaka 1984.

Katika vita vya Kagera mwaka 1979, akiwa Waziri Mkuu, Sokoine alikuwa kiungo muhimu, hata mwanzoni mwa vita hivyo, akiwaagiza wakuu wa mikoa wote wakusanye nyenzo zote tayari kwa vita ya kupambana na Nduli Idi Amin Dada wa Uganda.

Binafsi, mnamo Januari 23, 1979, akatembelea eneo la vitani mpakani Mutukula (sasa wilaya ya Misenyi) kukagua hali ya usalama na inaelezwa wakati wote wa vita, Sokoine alikuwa ni nadra kulala usingizi, hali inayotajwa hata kuchangia mtetereko wake kiafya.

Novemba 1980, kukafanyika uchaguzi nchini, Sokoine aliomba na kukubaliwa kujiuzulu uwaziri mkuu, akaenda nchini Yugoslavia kwenye matibabu, nafasi yake ikashikwa na Cleopa David Msuya.

Baada ya kurejea, Mwalimu Nyerere akamteua tena kuwa Waziri Mkuu Februari 24, 1983 na mwaka huo huo akiendeleza masomo yake ya Shahada ya Sayansi ya Siasa.

**MWASISI WA DALADALA**

Katika miaka ya 1980, nauli ya daladala ilikuwa Sh. tano na safari zake ni za 'kuiba', huku mitaa yote ikitawaliwa na mabasi rasmi ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

Kukua kwa jiji la Dar es Salaam, ikalemewa katika utoaji huduma. Sokoine akiwa Waziri Mkuu, akaamuru magari binafsi yaanze kuisaidia UDA kubeba abiri kwa nauli ya shilingi tano na kwa kuwa kiasi hicho cha pesa kimedumu kuwa na jina la mtaani 'dala' basi ikawa jina la mabasi binafsi 'Daladala.'

**VITA VYA UHUJUMU UCHUMI**

Aprili 5, 1983, Mwalimu Nyerere. Ndiye aliyezindua kampeni ya kupambana na wahujumu uchumi baada ya kupitishwa kwa sheria yake mwaka 1983, ambayo ikamea sana, ikiwamo kupitia redioni.

Ni sheria inayomtaka mtu aeleze mali zake, huku kukiwapo mahakama yake maalum, ambayo ilikuwa na vipengele vya masharti.

Utekelezaji wa kampeni hiyo, baadhi ya washukiwa katika sehemu nyingi nchini, hasa Dar es Salaam, walihofu sana na kutupa barabarani na mitaroni.

Hivyo ni vitu vya thamani vilivyoingizwa nchini kinyemela, kukiwapo simulizi ya kutupwa mabunda ya fedha na mali kama televisheni. Polisi wakaziokota na kuzikabidhi kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Ni wakati sheria za nchi hazikuruhusu mtu binafsi kuwa na maduka makubwa ya jumla, kazi iliyofanywa na Shirika la Biashara la Mkoa RTC

Ni rekodi iliyoacha, jina lake Sokoine likapaa maradufu hata kumjenga sana kisiasa, akapendeka zaidi kitaifa.

• ***Kwa mujibu wa ushuhuda, historia na michango ya uchambuzi.***

## Sokoine; safari yake alikotoka, hadi alikoishia na makuu aliyoyaacha

**INATOKA UK.11**

Ni Sokoine huyo anayeingia katika orodha ya kutunza na kutukuza utamaduni wa Kiafrika na utaifa wake Mtanzania, ikitimia miaka 40 tangu afariki dunia kwa ajali mkoani Morogoro.

Hilo ni tukio lililomkuta safarini, akitoka Dodoma bada ya kumaliza vikao vya bunge, akienda Dar es Salaam, huku akisimama njiani kuona maendeleo ya mashamba ya wakulima.

**HISTORIA YAKE**

Sokoine alizaliwa Agosti mosi mwaka 1934, katika wilaya ya Masai Land wakati huo, ambapo kwa sasa inafahamika wilaya ya Monduli, mkoani Arusha.

Baadaye, historia yake inaonyesha akapata elimu ya msingi, kati ya mwaka 1949 hadi 1953 akianzia Shule ya Msingi Monduli na kisha akajiunga na Monduli Middle School kuanzia mwaka 1953 hadi 1956.

Inatajwa, baada ya hapo mwaka 1957 akajiunga na shule ya Sekondari ya Umbwe, mkoani Kilimanjaro alikohitimu mwaka 1960.

Mnamo Januari Mosi,1961, Edward Moringe Sokoine akajiunga na chama cha Tanganyika African National Union (TANU), ikiwa ni miezi michache kabla ya Tanganyika haijapata Uhuru.

Baadaye mwaka 1962, Sokoine akapata nafasi ya kwenda nchini Ujerumani alikokuwa masomoni hadi 1963, akisomea uongozi na utawala.

Sokoine aliporejea nchini, akateuliwa kuwa Ofisa Mtendaji wilaya ya Maasai Land. Kutokana na uchapa kazi wake uliotukuka wilayani Monduli, wananchi wakamshawishi na hatimaye wakamchagua kuwa mbunge wao.

**AUTWAA UWAZIRI**

Kimsingi, ufanisi wake kiutendaji ulizidi kuonekana machoni mwa watendaji wakuu wa serikali, hata mwaka 1967 Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, akamteua kuwa Naibu wa Waziri wa Mawasiliano na Usafiri, nyota yake ya uongozi ikizidi kung'aa.

Mwaka 1972 akapandishwa daraja waziri anayehusika na usalama, huku msaidizi wake wakati huo , Marehemu Mzee Mhagama, akimwagia sifa za wakati huo, kwa stadi yake ya kufuatilia ahadi zake kikazi.

Marehemu Mzee Mhagama, akafafanua katika mizunguko yao kufuatilia majukumu, Sokoine alikuwa na kawaida akiahidiwa jambo, alikuwa na umahiri kifuatilia ahadi anayopewa kupata hatima inayofuata na yu mgumu kusahau.


Mwaka 1977, Sokoine akateuliwa kuwa Waziri Mkuu katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, akiwa mpenzi wa karibu wa siasa ya Ujamaa wakati huo.

Baadaye, akaiomba ruhusa kwa Baba wa Taifa aende masomoni nje ya nchi kuongeza ujuzi na akaruhusiwa kwenda masomoni na kurejea mwaka 1983, akateuliwa tena kuendelea na nafasi yake ya uwaziri mkuu.

Katika kikundi hicho cha mabadiliko, Rais Nyerere, akamteua Cleopa Msuya kushika nafasi hiyo. Kurejea kwake, Sokoine akaanzisha vita dhidi ya uhujumu uchumi nchini, akaudumisha hadi kifo chake asubuhi ya siku kama ya leo, ikitimu sasa miaka 40, wakati huo umri wa Sokoine ilikuwa miaka 46 tu.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

### Hili la kulipana posho tofauti linafikirisha






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

WAFANYAKAZI wa kipato cha chini baadhi yao kama si wote, wanapojikuta wamealikwa semina, warsha au kongamano, hujisikia vema sana. Si kwa sababu wanakwenda kupata maarifa mapya, bali kutunisha mifuko.

Hiyo inatokana na ukweli kuwa, mikusanyiko hiyo ya kitaaluma, huendana na malipo ambayo hujulikana kama posho ya kikao, ingawa ni wachache sana kama asilimia 0.01 ndio hufikiria zaidi maarifa kuliko kipato.

Na hiyo hutokea pia hata kwa wenye kipato.

Ndiyo sababu watu husema pesa ni kila kitu, ni sabuni ya roho, na bila hiyo hakika maisha huenda harijojo na ndiyo sasa tulivyozoea, bila

posho kwenye semina, warsha au kongamano, ni nadra kukuta ukumbi umesheheni, isipokuwa kama kuna kitisho kutoka kwa wakubwa.

Ndiyo sababu nakumbuka akiwa madarakani, 'meti' wangu, Daktari John Magufuli, alipata kupiga marufuku mikusanyiko hiyo, akisema ni ubadhirifu wa fedha za umma, akitaka watu waishi kwa mishahara.

Watu moyoni hawakufurahia hilo na akafika hata mahali akasema hata ukitaka kusafiri nje ya nchi, lazima upate kibali cha Ikulu, vinginevyo utaula wa chuya na kibarua kuota nyasi au kitumbua kuwekwa mchanga.

Hili jambo la posho limekuwa likinifikirisha sana, lakini baadaye nikiamini kuwa lazima liwepo, kwa sababu watu hata wakisikia wamepata safari mikoani, ndipo wanapoamini wanaweza kumalizia matatizo yao ya kifedha ikiwa ni pamoja na kulipa ada za watoto.

Inaeleweka, posho si mshahara, kwani mtu akifanyiacho kazi huwa ni mshahara na ndiyo sababu huheshimiwa, isikatwe kwa namna yoyote ile tofauti na posho, ambayo huweza kukatwa muda wowote kutokana na sababu mbalimbali.

Posho hutolewa kulingana na wadhifa au nafasi aliyo nayo mtu katika ajira yake na huweza kupanda kutokana na muktadha na kupungua kutokana na hali hiyo hiyo. Pia, inaweza kufutwa isiwapo kabisa na mtu akaendelea kuishi kwa mshahara.

Ndiyo sababu nasema, posho ni almasi kwa mfanyakazi wa kipato cha chini, kwani humsaidia sana kuziba mapengo ya kiuchumi aliyo nayo.

Hata hivyo, tumekuwa tukitofautiana katika kulipana posho hizi, kutokana na kazi tuzifanyazo.

Nimekuwa nikifikiria, mwalimu mathalan, kwa kazi na majukumu aliyo nayo ya kuandaa kazi, maazimio ya kazi, kufundisha na hatimaye kusahihisha madaftari ya wanafunzi, bila shaka hakuna posho anayolipwa na akidai, ataambiwa hiyo ni kazi yake aliyoisomea.

Mwanajeshi, sijui kama aendapo vitani kuna posho analipwa zaidi ya mshahara wake wa kila mwezi. Pengine nitaelimishwa, lakini sikusikia wanajeshi wetu katika miaka ya sabini waliponda Uganda kupambana na majeshi ya Nduli Dyamini kama walilipwa posho kila siku. Nitaelimishwa!

Madaktari wetu nasikia wao huwa wanalipwa posho kulingana na wagonjwa wanaoonana nao na ndiyo sababu kuna malipo ya kuonana na daktari nje ya mshahara wake wa kila mwezi.

Hujiuliza ni kwanini hilo linakuwa hivyo, wakati daktari ana mshahara? Wabunge wetu nao huwa naambiwa wana mishahara tena minono, lakini

bado kila wakikutana bungeni kuuliza na kujibiwa maswali au kuchangia hoja na kutunga sheria, hulipwa posho kila siku iitwayo ya 'kikao cha Bunge!'

Hata wasipokutana bungeni, wakiwa katika ziara za kamati zao, kukagua miradi au mashirika na taasisi za umma, bado hulipwa hizo posho na si za kitoto.

Lakini, wote hawa wamefundishwa na mwalimu masikini asiye na posho, afanyapo kazi yake kama ilivyoainishwa hapo juu, bado huishi kwa mshahara wake huo huo wa kijungujiko, huku anayestahili kumtetea mwalimu akilipwa mshahara na posho hapo hapo!

Kwani kigezo ni kipi kwa daktari kustahili posho ya kuonana na mgonjwa mbunge kukaa kikaoni kama kazi yake, huku mwalimu hana posho ya kuonana na mwanafunzi wake? Polisi hana ya kuonana na mhalifu?

Askari wengine nao nasikia nao hawana posho ya kuonana na mfungwa au wa Zimamoto kutolipwa posho ya kwenda eneo la tukio la moto au uokozi? Tuangaliane katika hizi posho jamani!

# Wadau sekta ya utalii wailililia halmashauri tozo kuongezeka

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

WADAU wa utalii wameilalamikia serikali tozo nyingi kwa watalii hasa dola 10 za Kimarekani wanazolipa katika mageti ya halmashauri na kusababisha wageni wanaotembelea hifadhi kukata tamaa kabla ya kufika katika vivutio.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwa niaba ya wenzake, Mwenyekiti wa waongoza utalii Kanda ya Kaskazini, Engelbert Qorro, alisema ni muhimu Mkuu wa Mkoa, Paul Makonda, akaanza na kero hiyo na miundombinu ya hifadhi ili watalii wasiendelee kuteseka.

"Waachane na kodi wanazowatoza watalii barabarani hizi halmashauri zinapata fedha kutoka TAMISEMI halafu serikali inakusanya mapato kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na zenyewe zina mgao wake ambao unaenda halmashauri wao wanakusanya ya kazi gani ni changamoto kubwa inatutesa," alisema.

Alisema inapoonekana utalii unashamiri kwenye ukanda wa Kaskazini wanaweka tozo nyingi hadi mgeni anakasirika kabla ya kufika kwenye hifadhi kwa kuwa anajikuta ameshalipa fedha nyingi na mambo mengine sio ya msingi.

"Unatoka hifadhi fulani kwenda nyingine kuna hao ndege wanaitwa flamingo sasa wanapoenda kutembelea maeneo yale unakutana na geti za halmashauri ambazo zinaleta sitofahamu kwa wageni kila geti wanachaji dola 10 za Kimarekani na geti la mwisho ni dola 35 kwa kichwa wakati hili eneo lipo chini ya TAWA na hawa TAWA wanalipisha dola 29.5 za Kimarekani ambapo ni sahihi tunatamani hawa wangefanya hiyo kazi kuliko halmashauri."

Alisema wanapotembea na wageni kuangalia flamingo kuna kijiji kinategemea kila mtalii kulipa dola 20 za Kimarekani na bado kuna malazi, hivyo anajikuta analipa dola 85.

"Njia nzima mgeni anaangalia ng'ombe, mbuzi na kondoo sasa wanashangaa kwanini wanadaiwa fedha nyingi wakati shida yao ni kuangalia flamingo, naishauri serikali ili kupunguza ule uchungu wa Tanzania gharama tupunguze hizi kodi ndogo ndogo ndio zinasumbua wageni hasa hizi dola 10 za kwenye mageti ya halmashauri," alisema Qorro.

Alisema dola 10 wanazozitoa kwenye Halmashauri hazina maana kama serikali inarudisha asilimia 50 kwenye vijiji ama kwenye halmashauri akitolea mfano Wilaya ya Longido, Monduli na Ngorongoro, TAWA inakusanya dola 29.5 za Kimarekani kwa mgeni mwisho wa mwaka wanarudisha kwenye hizo halmashauri.

"Sasa kuna haja gani ya halmashauri kukusanya kodi kutoka kwa wageni hapo ndipo watalii wetu wanapochanganyikiwa tujitahidi kupunguza hizi tozo ili tufikie malengo ya kuwapata watalii wengi zaidi," alisema.

Pia, alisema barabara za hifadhi ni mbovu na vyombo vya kutengeneza vipo, lakini wanashindwa kuelewa kwanini zinapoharibika hazitengenezwi kwa wakati na kusababisha usumbufu kwa watalii.

"Barabara zetu ndani ya hifadhi hazifai kuna mashimo makubwa huwezi hata kupishana na mwenzako. Watalii wengi ni wazee wanakuja kupumzika katika hifadhi tunapowapitisha katika hizo barabara mbovu wanalalamika na wengine kunashindwa kuendelea na usafiri wa magari na kuagiza ndege imfuate huyu atakaporudi nchini kwake anaweza kusababisha tukakosa wageni kuja kwa namna atakavyoelezea miundombinu ya barabara, " alisema Qorro.

Alisema wanaiomba serikali kurudisha mafungu kwa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaha ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA) ili inapotokea matatizo wayashughulikie kwa wakati badala ya kusubiria fedha itoke serikalini kwa kuchelewa na tatizo kuzidi kuongezeka.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto), akizungumza na Kada wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Mkuu wa Mkoa mstaafu, Mzee Stephen Mashishanga alipomtembelea kwa ajili ya kumjulia hali nyumbani kwake, Mtaa wa Forest, Manispaa ya Morogoro jana. **PICHA: ONWM**

## RC Kunenge abana viongozi matumizi ya rasilimali misitu

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

MKUU wa Mkoa wa Pwani ameagiza viongozi wa vijiji kuhakikisha wanapouza maeneo, wasiingilie misitu hata kama haihifadhiwi kisheria.

Abubakar Kunenge pia ameelekeza viongozi wa wilaya, Halmashauri na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) wahakikishe misitu iliyohifadhiwa inatunzwa kwa kuzuia shughuli za kibinadamu ukiwamo ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa, uvamizi wa mifugo, uchimbaji michanga, kokoto kilimo na makazi.

Alitoa maelekezo hayo juzi mjini Kibiti wakati wa maadhimisho ya Siku ya Upandaji Miti Mkoa wa Pwani, maagizo hayo yakisomwa na Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo.

Alisema ongezeko la watu na ukosefu wa nishati vimetoa msukumo wa mahitaji ya mazao ya misitu ikiwamo kuni, mkaa na maeneo ya makazi na hivyo kusababisha kuongezeka ukataji miti na ufyekaji misitu.

Alisema serikali za vijiji, wilaya, halmashauri na taasisi nyingine zikisimamia maelekezo hayo, zitaimarisha ulinzi na usimamizi wa misitu kwenye maeneo yao.

Maelekezo mengine yaliyotolewa ni pamoja na kila halmashauri kupeleka taarifa ya maendeleo ya miti iliyopandwa mwaka 2022/23 na kueleza sababu za miti mingine kunyauka baada ya kupandwa.

Kanali Kolombo alibainisha kuwa kwa kipindi hicho, Mkoa wa Pwani ulipanda miti 8,876,640 na katika msimu huu wa 2023/24, miche 10,436,494 imezalishwa na inaendelea kupandwa katika maeneo mbalimbali mkoani humo.

"Kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, ninawasilisha maelekezo haya ya kila halmashauri kuhakikisha wanafikia malengo ya serikali ya kupanda miti milion 1.5," alisema Kanali Kolombo.

# TANROAD wapiga kambi kutengeneza barabara korofi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Morogoro umeweka kambi ya wahandisi wilayani Kilombero ili kufanya kazi usiku na mchana za matengenezo ya barabara kwenye maeneo korofi kurejesha huduma za mawasiliano na usafiri katika maeneo yanayounganisha wilaya hiyo na nyingine.

Mpango huo utaziwezesha kupitika kipindi chote cha mwaka katika barabara yenye urefu wa kilometa 150 kutoka Ifakara hadi Mlimba.

Meneja wa Mkoa wa Wakala huo, Mhandisi Alinanuswe Kyamba, alisema hayo wakati akizungumzia mkakati wao wa kuhakikisha barabara zinazohudumiwa na wakala huo zinapitika nyakati zote hasa kwa kipindi hiki cha mvua katika maeneo mbalimbali nchini.

Mhandisi Kyamba alisema, maeneo mengi ya barabara ndani ya mkoa zimekumbana na changamoto kwa kipindi hiki ambacho mvua inaendelea kunyesha ikiwamo barabara ya Ifakara – Mlimba kwa baadhi ya maeneo kukatika.

"Ipo tayari timu ya wahandisi wetu wilayani Kilombero ili kuyafikia maeneo yote korofi na kufanya matengenezo kurejesha mawasiliano ya barabara kwakuwa ndio kitivo cha uchumi katika suala la kilimo," alisema Mhandisi Kyamba.

Alisema kampuni tatu za kutengeneza barabarara tayari zipo wilayani Kilombero kurekebisha maeneo yote korofi na kazi hizo zinafanyika usiku na mchana.

"Lengo letu ni kuona barabara ya Ifakara – Mng'eta hadi Mlimba inafunguka kwa wakati na inapitika muda wote," alisisitiza Mhandisi Kyamba.

Baadhi ya wananchi na wafanyabiashara, akiwamo Libonge Mkalimoto, mfanyabiashara mjini Ifakara alisema kukatika kwa mawasiliano ya barabara hiyo kumechangia kupanda kwa bei ya bidhaa na ongezeko la nauli.

Mkalimoto alisema magari yanayotoka Ifakara kwenda Mlimba zaidi ya kilometa 150, yanalazimika kukoma eneo la Mng'eta kutokana maeneo yake tofauti kukatika kutokana na mvua.

Shukuru Liguguda, mfanyabiashara eneo la Lumemo alisema, wasafiri wa njia hiyo wanalazimika kutumia pikipiki (bodaboda) na kulipa hadi Sh. 40,000 kutoka yanapokoma magari eneo Mng'eta ili kwenda Mlimba.



# PPRA yabaini ununuzi kutofuata sheria

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), imebaini katika matumizi ya taratibu ya ununuzi kwa njia ya 'force account' hayaendani na sheria na kanuni za ununuzi zinavyoelekeza.

Aidha, ushiriki wa kampuni za biashara zinazoongozwa na wanawake katika zabuni za umma umebainika kukabiliwa na kikwazo cha kushindwa kupata dhamana ya zabuni inayotakiwa.

Akizungumza juzi jijini hapa, Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri na Kujenga Uwezo kutoka Mamlaka hiyo, Amini Mcharo, alisema hali hiyo imebainika katika utafiti uliofanywa na mamlaka hiyo zilizolenga kubaini vikwazo vya sekta ya ununuzi na kutafuta suluhisho.

Alisema kutokana na hali hiyo sheria mpya ya ununuzi ya mwaka 2023 imeboresha utaratibu huo na kuweka upendeleo maalum kwa kampuni za wanawake.

Kuhusu kuongeza ukaguzi na uokoaji wa fedha za umma, Mcharo alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan mamlaka hiyo ilifanya uchunguzi wa zabuni zilizotekelezwa kwa mwaka 2021/22 na 2022/23 na kuokoa fedha za umma Sh.Bilioni 16.27.

Alifafanua kuwa kati ya fedha hizo Sh. bilioni 13.83 ilitokana na kuingilia kati mamlaka kwenye mikataba ambayo ilitolewa kwa wazabuni wenye bei ya juu wakati wenye bei ya chini wakitolewa kwenye mchakato.

Pia, alisema kati ya fedha hizo Sh. bilioni 2.44 kilichorudishwa na wasambazaji wa bidhaa na wakandarasi kwa malipo ya ziada yaliyofanywa na taasisi za ununuzi.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri akizungumza na wafanyabishara wa soko la wazi la Machinga, jijini Dodoma juzi, kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na usafi wa mazingira. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# VETA kuwajengea uwezo wafanyakazi majumbani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIKA kuimarisha utendaji kazi wa wafanyakazi majumbani, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na shirika lisilo la kiserikali la watu wanaojitolea ulimwenguni (CVM), wameanzisha mitaala ya kuwajengea uwezo ili kuleta ufanisi wanapotekeleza majukumu yao.

Akizungumza kwenye makabidhiano ya mitaala ya kozi hiyo ambayo itachukua kati ya mwezi mmoja hadi miezi sita, Ofisa Mkuza Mitaala wa VETA, Anna Nyoni, alisema shirika hilo lilifanya utafiti kwa wafanyakazi wa majumbani na kugundua wengi wanafanya kazi bila kuwa na ujuzi na kuona kuna haja ya kutoa mafunzo kwa na mahali pekee walipoona panafaa kujengewa uwezo ni chuo hicho.

"Mtaala huu tumeuandaa kutoka kwenye kozi zinazotolewa na VETA kama vile ya upishi na usafi ambapo tuliona kuna vitu vingine zaidi ya upishi na usafi ambavyo wanavihitaji kama vile ya kuwalea watoto na wazee pamoja na baadhi ya huduma za majumbani kwa wale wanaoenda kufanyakazi nje ya nchi," alisema.

Alisema kwa kuwa mtaala ni mpya, wametoa mafunzo pia kwa walimu 12 ambao watawaelimisha wanafunzi wa kozi hiyo kwenye vyuo vyenye mradi ikiwamo mikoa ya Dodoma, Iringa, Dar es Salaam, Tanga na Lindi na Morogoro.

Alisema pia vifaa kwa ajili ya kufundishia kozi hiyo vimeshaandaliwa ili kuwajengea uwezo wafanyakazi wa majumbani wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi na ndani.

Naye, mtaalam wa jinsia kutoka shirka la CVM, Maria Shimba alisema kwa wafanyakazi ambao hawatakuwa na fedha za kulipia mafunzo hayo watakopeshwa na baada ya kupata kazi watarejesha na kwa ambao wana uwezo wa kujigharamia wataendelea na masomo kwa utaratibu utakaotolewa na VETA.

Alisema mafunzo hayo kwa wafanyakazi wa majumbani yatawapa ujuzi kama ilivyo kwenye kozi nyingine na watatambulika kwa vyeti vyao kutoka VETA kama ilivyo kwenye udereva na kuwasaidia kupata ajira kwa kuwa na leseni za chuo hicho.

# Wanafunzi wahadharishwa matumizi dawa za kulevya

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida, imewatahadharisha wanafunzi wa vyuo vikuu mkoani hapa kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya na rushwa kwani vinawaharibu vijana ambao ndio hazina ya taifa.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Sipha Mwanjala, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi kutoka Chuo cha Maji, Chuo cha Afya, Chuo cha Utumishi na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida katika kongamano lililoandaliwa na TAKUKURU lililohusu rushwa na dawa za kulevya.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kuwaongezea uelewa wa mapambano dhidi ya rushwa na dawa za kulevya kwa kuwa kundi la vijana ndilo lipo katika hatari zaidi ya kuathirika na vitendo hivyo.

Mwanjala alisema TAKUKURU imeamua kuwashirikisha vijana katika kongamano hilo kwa sababu inatambua vijana ni mtaji usiofilisika na ni hazina ya taifa hivyo wakipata elimu ya rushwa watasaidia kuzuia na kupambana na rushwa kwa kutoa taarifa TAKUKURU na kuwa mabalozi kwa wenzao ambao hawakupata elimu hiyo.

Aliongeza kuwa vijana ni kizazi na wazazi wa kesho hivyo wakijua umuhimu wa maadili na kuepukana na vitendo vya rushwa TAKUKURU inaamini watawafundisha watoto wao kufuata sheria, kanuni na taratibu kuepukana na rushwa hali ambayo itasaidia kupunguza kama sio kumaliza kabisa tatizo la rushwa nchini.

"Kunapokuwa na rushwa hakuna maadili na kukiwa na maadili hakuna rushwa,hivi sada vijana wapo vyuoni na keshokutwa wao ndio watakuwa maofisini hivyo wakielimishwa na kutambua maadili watafanya kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu na watatenda haki na wananchi watapata huduma stahiki," alisema.

Naye Mratibu wa TAKUKURU na Skauti Mkoa wa Singida, Faruma Nkumbi, alisema wao kama wadau ni muhimu kuwapa elimu vijana kwasababu kundi hilo ni taifa la leo na kesho ambao kama litajiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya nguvu kazi itapungua na uchumi wa taifa utadorora.

Ofisa Vijana Mkoa wa Singida, Frederick Ndahani, aliwataka vijana kuwa wazalendo na kuacha tamaa ya kuwa na maisha mazuri kwa haraka kwani vitendo hivyo ndio kichocheo kikubwa cha wao kujiingiza katika vitendo vya rushwa na dawa za kulevya.

Wanavyuo hao walisema elimu waliyopewa ya rushwa na dawa za kulevya itawasaidia sana kuepuka na vitendo hivyo ambavyo pengine baadhi yao walikuwa wakivifanya kutokana na kutokuwa na elimu ya masuala hayo.





# Kambi rasmi matibabu ya magonjwa sugu yaandaliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa kushirikiana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa, imeanzisha kambi maalumu ya matibabu ya kibingwa kwa watu wenye matatizo ya mishipa ya fahamu, ubongo na saratani.

Kambi hiyo inawahusisha madaktari bingwa kutoka katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambao mbali na kutekeleza jukumu hilo, pia wanawaongezea uzoefu madaktari waliopo katika hospitali ya kanda ya Mbeya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alisema kambi hiyo ni ya siku nne na ilianza Aprili 8 mwaka huu na inatarajiwa kufikia tamati leo ambapo wananchi wanafanyiwa uchunguzi bure na kufanyiwa upasuaji.

Alisema baada ya kukamilika kwa kambi hiyo matibabu hayo ya kibingwa yataendelea ili kuhakikisha wananchi wote ambao wana matatizo hayo wanahudumiwa.

"Tunashirikiana na chama cha madaktari bingwa wa mishipa ya fahamu na ubongo kutoka MOI, kwahiyo tunawashauri wananchi wenye matatizo hay ana hata ndugu wenye watu wao ambao wana matatizo wawalete ili wahudumiwe," alisema Dk. Mbwanji.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile, alisema lengo la kuweka kambi hiyo ni kuwapunguzia wananchi gharama za matibabu ya kibingwa ambayo walitakiwa wayafuate Dar es Salaam.

# Mgogoro binadamu, wanyamapori washika kasi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MIGOGORO ya wanyamapori na binadamu imeanza kushika kasi mkoani Mbeya kutokana na mwingiliano wa shughuli za kibinadamu na wanyama hao.

Ndani ya wiki mbili sasa, watu wanne wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa kwa kushambuliwa na wanyama hao.

Tukio la kwanza lilitokea katika kitongoji cha Gengeni, Kata ya Kambikatoto, wilayani Chunya. Katika tukio hilo, watoto watatu wa familia moja walifariki dunia kwa kushambuliwa na fisi huku wazazi wote wawili wakijeruhiwa.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Abdi Issango, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 7, mwaka huu. Alisema fisi huyo alitokea katika Pori la Akiba la Rungwa na kuwavamia wanafamilia hao usiku.

Aliwataja watoto waliofariki dunia kwenye tukio hilo kuwa ni Samweli Shigela (5), Kasunzu Shigela (3) na Ngasa Shigela mwenye umri wa mwaka mmoja, wote wakazi wa kitongoji cha Gengeni.

Issango aliwataja wazazi waliojeruhiwa na mnyama huyo kuwa ni Shigela Ngasa (45) na mkewe, Limi Masanja (38) ambao walikumbwa na madhara hayo wakati wakipambana na kujiokoa na kuokoa watoto wao.

Alisema majeruhi wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Mtakatifu Gasper, Itigi wilayani Manyoni, Singida ambako walipelekwa baada ya kuokolewa.

"Fisi huyo alifanikiwa kuingia kwenye nyumba hiyo kutokana na kutokuwa na mlango na iko porini karibu na hifadhi. Baada ya kuwaua watoto hao na kuwajeruhi wazazi, aliua kondoo watatu na kisha akakimbilia porini," alisema Kamanda Issango.

Hata hivyo, alisema siku ya pili fisi huyo alirejea katika eneo hilo na ndipo Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na maofisa wanyamapori kutoka katika pori hilo la Rungwa walimwua.

Katika tukio lingine, mtu mmoja anadaiwa kuuawa kwa kuliwa na Simba huku kijana wa miaka 14 akijeruhiwa kwa kukanyagwa na tembo katika wilaya ya Mbarali. Inadaiwa kuwa wanayama hao wanatokea katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.



Baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Kilambo, Kata ya Kikusya wilayani Kyela mkoani Mbeya, wakiwa wameshika miche ya miti na wanafunzi wa shule hiyo ambao ni wanachama wa Klabu ya mazingira, wakati wa uzinduzi wa upandaji miti shuleni hapo, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafanyabiashara ndogondogo Mbeya wapewa mchongo mikopo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wadogo, maarufu kama Machinga, ambao wamekuwa wakifanya shughuli zao kwenye maeneo yasiyo rasmi yakiwamo hifadhi za barabara, wameshauriwa kuhamia kwenye masoko rasmi ili wanufaike na fursa mbalimbali ambazo zinatolewa na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alitoa ushauri huo juzi kwenye uzinduzi wa mpango maalumu wa mikopo bila dhamana kwa wafanyabiashara walioko katika maeneo rasmi, wakiwamo walioko kwenye masoko jijini Mbeya. Mpango huo umeanzishwa na benki ya CRDB.

Alisema ili kuwaepusha wafanyabiashara hao na adha mbalimbali, serikali imewapangia maeneo ambayo yameandaliwa yakiwamo masoko lakini bado wanaonekana wakirandaranda kwenye maeneo ya barabarani.

Eneo la uwanja wa zamani wa ndege wa Mbeya, alisema limetengwa eneo maalumu kwa ajili ya machinga na baadhi yao wamejenga vyumba vya biashara na wanaendelea na shughuli zao bila bughudha.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea kuboresha miundombinu mbalimbali zikiwamo barabara ili kuruhusu magari kuingia kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kupeleka bidhaa na abiria ambao ndio watakuwa wateja wao.

"Hii ni fursa muhimu kwenu wajasiriamali wetu. Ingieni kwenye masoko hayo mfanye kazi zenu na mpate pia fursa ya mikopo yenye masharti nafuu katika orodha ya masoko hayo hata soko hili la uwanja wa ndege limo," alisema.

Malisa alisema pamoja na hamasa ambayo imeanzishwa na benki ya CRDB lakini kuna mpango wa kuanza kuwaondoa wafanyabiashara hao kwa nguvu kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi.

Meneja Masoko wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Japhar Hasanali, alisema lengo la kuanzisha mpango huo ni kuwaepusha wafanyabiashara hao na mikopo inayotolewa na taasisi zisizo rasmi ambayo ina riba kubwa maarufu kwa jina la 'kausha damu'.

Alisema wanakusudia kuwafikia wafanyabiashara wote wadogo wanaofanya shughuli zao kwenye maeneo rasmi ili kuhakikisha wanawainua kiuchumi na kwamba sharti pekee la mikopo hiyo ni mfanyabiashara kuwa kwenye eneo rasmi hasa sokoni.

Mikopo wanayotoa, aliema haijalishi aina ya biashara ambayo mhusika anafanya badala yake ni wanataka awe kwenye eneo rasmi la kufanyia shughuli zao.

"Tumetambua kwamba kuna baadhi yenu wanakwenda kuchukua mikopo kwa watu binafsi ambao wanawatoza riba kubwa, mnajikuta badala ya kujiinua mnawafanyia kazi wao, sasa sisi tumekuja na suluhisho la mikopo hii yenye mashart nafuu kabisa," alisema.

Mwenyekito wa Jumuiya ya Masoko ya Jiji la Mbeya, James Mwaikambo, aliiomba serikali kutotumia nguvu kuwaondoa wamachinga barabarani na badala yake hekima itumike ili kuepusha kuumizana na kuharibu biashara.

Alisema serikali inatakiwa iendelee kuboresha masoko na maeneo mengine rasmi ili yawavutie wafanyabiashara kwenda na hivyo kumaliza tatizo la uvamizi wa barabara.



# Mahakama: Sheria ya Vileo inakinzana na Katiba ya Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Zanzibar imesema Sheria ya Vileo Na. 9 ya Mwaka 2020 inayozuia kampuni zaidi ya tatu kuingiza pombe Zanzibar, inakwenda kinyume cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Ufafanuzi huo umekuja baada ya kampuni ya Quality Meats and Beverage (QMB) supplies LTD kufungua shauri mahakamani kuomba tafsiri ya kikatibamwishoni mwa mwaka jana

Jaji wa Mahakama Kuu, George Joseph Kazi alieleza kuwa baadhi ya vifungu hasa cha 33 (1) cha Sheria Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020 ni kinyume na Katiba.

Kifungu hicho kinazuia utoaji wa leseni za biashara ya pombe kwa kampuni zisizozidi tatu na kwamba ni kinyume na Sheria ya Ushindani Sawa na Kulinda Mlaji Namba 5 ya Mwaka 2018 yenye vipengele vinavyotoa uhuru wa kibiashara iliyotungwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Katika uamuzi huo wa Aprili 4 mwaka huu, Jaji Kazi alisema kifungu hicho cha 33 ya sheria ya vileo ni kinyume na Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 vifungu kadhaa ikiwemo cha 12, 13, 21 na 22.

"Mahakama inatoa uamuzi kuwa kukataa au kunyimwa kwa leseni kwa kampuni inayolalamika ni kinyume cha sheria, na uwamuzi huo ni batili," Jaji Kazi alisisitiza katika uwamuzi wake.

Mahkama pia ilimtaka Mrajis wa Mahakama Kuu akabidhi utaratibu wa mauzo, mlalalamikaji, makontena yaliyoletwa eneo Mahakama na kitengo cha mnada mahakama na makontena yote ambayo hayajauzwa na yaliyokuwa yakishikiliwa, arejeshewe.

Aidha, Mahakama ambayo kwa mara ya kwanza ilitoa uamuzi Machi 19 mwaka huu kabla ya Aprili 4 mwaka huu, ilimtaka mlalalmikaji alipe Bodi ya Vileo ada ya leseni ya uingizaji wa pombe kutoka nje, kwa mwaka 2022.

Shauri hili linatokanana na mlalamikaji (Quality Meats and Beverage-QMB supplies LTD) kuwasilisha katika Mahakama Kuu malalamiko dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, mshitakiwa au mlalamikiwa wa pili, baada ya kunyimwa leseni ya kufanya biashara ya kuingiza na kusambaza pombe Zanzibar.

Katika shauri hilo kampuni hiyo (mlalamikaji) iliomba Mahakama Kuu isikilize na itoe tamko kuwa: Baadhi ya vifungu katika Sheria ya Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020 ni kinyume na Katiba ya Zanzibar; na kuwa Sheria ya Ushindani wa Kibiashara na Kumlinda Mlaji ambayo inatoa uhuru wa kufanya biashara iheshimiwe.

Mlalamikaji pia aliomba Mahakama Kuu ya Zanzibar itoe maelekezo kuwa walioathika na kupata hasara kutokana na utekelezaji wa sheria ya vileo, wawe huru kufanya biashara zao wakati ikisubiriwa kurekebisha upya sheria ya vileo ili iwe rafiki na isitoe kikwazo chochote katika ushindani sawa wa biashara hiyo; na pia Mahakama itoe uamuzi wowote ambao itaona unafaa katika kutoa haki ya kibishara hiyo.

Mlalamikaji aliwasilisha sababu 13 za kupinga Sheria ya Vileo ya Mwaka 2020 na baadhi ya vipengele vyake na kwamba ni kinyume na Katiba ya Zanzibar ambayo imetoa uhuru wa kufanya biashara.

Walalamikiwa, Mwanasheria Mkuu aliwakilishwa na mwanasheria Sarah Khatau, na TRA iliwakilishwa na mwanasheria Maryami Ali, ambao kwa nyakati tofauti walipinga madai yaliyowasilishwa na mlalamikaji.

Mawakili au watetezi wa walalamikiwa walitaka shauri litupwe na Mahakama Kuu kwa madai kuwa hakidhi vigezo na linakosa uzito wa kisheria, lakini wakati wa usikilizaji wa shauri hilo mlalamikiwa wa kwanza aliondoa pingamizi ya kuataka shauri litupwe na Mahakama.

Lakini ili kuepuka kuchelewesha shauri hilo, jaji aliagiza wahusika wandae vizuri sababu zao kimandishi juu ya sababu za kupinga na kuwasilisha au kutowasilisha shauri hilo.

Serikali ya Zanzibar kupitia Bodi ya Vileo ilifanya marekebisho ya Sheria ya Vileo ya Mwaka 2020 na kuweka sharti kuwa ni kampuni tatu tu ndizo zinazoruhusiwa kuangizia pombe kutoka nje na kuingiza ndani ya Zanzibar.

Wakati sheria imeanza kutekelezwa, mlalamikaji alikuwa tayari ameagiza pombe kutoka nje ambayo ililetwa na kuzuiliwa katika Bandari ya Zanzibar na baadae kupigwa mnada na TRA baada ya kushindwa kutoa bandarini kutokana na kunyimwa leseni.

Akizungumzia uamuzi wa Mahakama Mbunge wa zamani wa Kikwajuni, Parmuk Singh Hoogan, alisema maamuzi ya mahakama yanapaswa kuheshimiwa na mamlaka ya serikali ili kulinda Katiba ya Zanzibar.

Hatua ya Bodi ya Vileo Zanzibar kuzinyima kampuni tatu leseni za kuingiza vinywaji kutoka nje kumesababisha uhaba wa vileo Zanzibar tangu Januari mwaka huu na kuathiri sekta ya utalii Zanzibar.

# Serikali inathamini mchango wa sekta binafsi kusaidia yatima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Viti Maalum, Hudhaima Mbarak Tahir amesema serikali inathamini mchango unaotolewa na taasisi binafsi katika kusaidia watu walio katika mahitaji maalum, ikiwemo yatima na wenye ulemavu.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati wa chakula cha mchana, kilichoandaliwa na Jumuiya ya Majlis Almaarif Islamia kwa ajili ya watoto yatima wa eneo la Mtopepo na vijiji vya jirani, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Sikukuu ya Eid-El- Fitr.

Alisema kitendo kinachofanywa na baadhi ya taasisi binafsi kula chakula cha pamoja wakati wa sikukuu na futari wakati wa mwezi wa Ramadhani ni miongoni mwa kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha watoto hao hawatengwi na jamii.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kufuatilia nyendo za watoto wao ili kuwakinga na vitendo viovu, ikiwemo udhalilishaji sambamba na kuwataka watoto hao kutiii wazazi wao ili waweze kukuwa katika maadili mema.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Shekhe Tahir Khatib Tahir, alisema lengo la kuandaa chakula hicho ni kuwafurahisha watoto hao na kujihisi hawatengwi katika jamii.

Aidha, aliwataka watu wenye uwezo kujitokeza kuwasaidia ili kupata neem ana rehema za Mungu.



Mwakilishi wa Viti Maalum kupitia vijana, Hudhayma Mbarak Tahir akizungumza na watoto yatima wakati wa chakula cha mchana, kilichoandaliwa na Taasisi ya Majilis Almaarif Islamiyya, kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu ya Eid El Fitri, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: MAELEZO ZNZ**

# Mama Mwinyi ahimiza matendo mema baada ya mfungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi ameitaka jamii kuendeleza mema yote ya mwezi wa Ramadhani hata baada ya kumalizika kwa ibada za mfungo huo.

Aliyasema hayo, jana kwenye ziara yake ya kuwatembelea wazee, watoto yatima na jamii zenye uhitaji katika vituo mbalimbali vilivyopo ndani ya Wilaya za Unguja kwa lengo la kuwafariji na kuwapa mkono wa Sikukuu ya Eid-El Fitri.

Mariam Mwinyi ambae pia ni msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), alizungumza na watoto yatima wa vituo hivyo vilivyopo Fuoni Mambo sasa, Wilaya ya Magharibi A, Kijiji cha kulelea watoto yatima SOS, Mombasa - Wilaya ya Magharibi B pamoja na nyumba ya kuwatunzia watoto Mazizini Mkoa wa Mjini wa Mjini Magaharibi.

Aidha, Mariam Mwinyi aliwataka watoto hao kuendeleza tabia njema kwa kuendeleza ibada na mazuri yote wanayoelekezwa wa wakubwa wao.

Aliwataka walezi na walimu wanaowasimamia watoto hao kwa juhudi za kuwakuza vyema.

"Nafarajika sana kipindi hiki cha sikukuu nikiwa pamoja nanyi, kadri ninavyowaona mnafurahi nami, sikukuu yangu huanzia hapo, furaha yangu mimi ni kuwaona nyie mkiwa na furaha siku zote" alisema.

Akizungumza kwenye ziara hiyo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisifu na kupongeza ziara za Mariam Mwinyi kwa wazee na watoto hao na kueleza kuwa ziara hizo ni utaratibu aliojiwekea kila ifikapo mwenzi wa Ramadhani pamoja na sikukuu kuwatembelea na kufurahia nao.

Wazee na watoto hao walimshkuru Mariam Mwinyi kwa sadaka ya futari aliyowapatia kipindi cha Ramadhani pamoja na kujumuika nao wakati huu wa furaha ya Sikukuu ya Eid -El Fitri.

Wazee hao walisifu ushirikiano wanaoupata kutoka Wizara Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto kwa kuendelea kuwa karibu nao wakati wote.

Pia, wazee hao walimtakia kheri Rais Mwinyi na kumuombea neema kwenye majukumu yake ya kuiongoza Zanzibar.



Mbunge wa Jimbo la Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda (katikati), akimsikiliza Meneja wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) wa wilaya ya Mlele, Zebron Malima (kushoto), wakati akikagua nguzo za umeme zitakazotumika kwenye mradi wa ujenzi wa njia ya umeme kutoka Inyonga hadi Majimoto, katika halmashauri ya Mpimbwe, wilayani Mlele mkoani Katavi juzi. **PICHA: WANMM**

# Wahitimu 2,500 wa chuo kikuu kuwezeshwa mafunzo ughaibuni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kufungua fursa za kuongeza umahiri katika fani zao, Taasisi ya CRDB Bank Foundation kwa kushirikiana na Sokoine University Graduate Entrepreneurs Cooperative (SUGECO) wametia saini mkataba wa miaka mitatu kuwezesha zaidi ya wahitimu 2,500 wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano hayo jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa amesema kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa taasisi yake imekuwa inatekeleza Programu ya Imbeju inayotoa mafunzo ya ujasiriamali na mtaji wezeshi kwa vijana na wanawake.

Alibainisha kuwa tangu walipofungua dirisha la maombi mwaka mmoja uliopita, vijana 709 walijitokeza na kati yao, asilimia 40 walitoka katika sekta ya kilimo ambayo inaongoza kwa kuliingizia taifa fedha za kigeni huku ikilihakikishia taifa chakula cha kutosha kwa mwaka mzima.

Kwa kushirikiana na wabia, Tully alisema kilimo kinapewa msisitizo zaidi kwa kutambua mchango wake katika kuliingizia taifa fedha za kigeni, kutoa ajira kwa Watanzania pamoja na kuihakikishia Tanzania usalama wa chakula.

"SUGECO ni mbia wetu mpya katika uwezeshaji wa vijana hasa wanaojihusisha na kilimo. Kwa kutambua umuhimu wa mafunzo kwa vitendo katikakuwajengea uwezo vijana, CRDB Bank Foundation imetenga Euro milioni 24 sawa na Sh. bilioni 67 kwa ajili ya programu hii zitakazotolewa ndani ya miaka mitatu ya ushirikiano wetu na SUGECO ili kuwaandaa vijana mahiri watakaoajiria au kujiajiri kwenye sekta ya kilimo," alisema.

Tangu kuanzishwa kwake, SUGECO huwapeleka nje ya nchi wahitimu wa SUA hasa katika mataifa ya Ulaya, Amerika na Asia ambako hujifunza namna nzuri ya kufanya kilimo chenye tija, mchakato huo ukihitaji fedha za awali kumwezesha mhitimu husika kujiandaa ipasavyo.

Kwa mwaka huu wa kwanza, Tully alisema wanatarajia kuwawezesha zaidi ya wahitimu 2,500 kwa kati ya Dola 3,500 za Marekani (Sh. milioni 8.7) na Dola 4,500 (Sh. milioni 11.29) zinazotosha kwa mahitaji yao yanayojumuisha gharama za pasi ya kusafiria, visa pamoja na fedha ya kujikimu kabla ya kuanza kulipwa huko waendako.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUGECO, Revocatus Kimario alisema ushirikiano na Taasisi ya CRDB Bank Foundation utaongeza idadi ya wanufaika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa mwaka jana walipeleka vijana 500 tu kupata mafunzo hayo kwa vitendo nje ya nchi ili kupata elimu na kujengewa uwezo zaidi katika kilimo, fani ambazo wamezisomea.

"Ushirikiano huu, tunaamini utakuwa na tija kubwa kwani ili ufanye biashara endelevu ni muhimu kuwekeza kwa watu unaowahudumia. Mkataba huu ni kati ya uwekezaji mkubwa kwa Benki ya CRDB kwani si wahitimu peke yao watakaonufaika bali wafanyakazi wao, familia hata ndugu, jamaa na marafiki zao," amesema Kimario.

Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Bodi ya SUGECO, Dk. Anna Temu alikumbusha namna walivyouanzisha ushirika huo ambao mpaka sasa umeneemesha maelfu ya wahitimu wa SUA kwa kuongezea maarifa juu elimu waliyoipata darasani.

"Kwa kuwa sisi tunahudumia zaidi vijana na wanawake, tuliona CRDB Bank Foundation wenye Programu ya Imbeju ni wabia muhimu wa kufikisha malengo yetu kwa jamii," alisema Dk. Anna.

**KICHEKO WAKULIMA**

Katika hatua nyingine, Tully alisema kuwa kwa kushirikiana na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) watatoa Sh. milioni 750 ambazo zitatumika kama mitaji wezeshi kwa vikundi na wakulima wadogo wa zao la shahiri katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha.

"Mpaka sasa Sh. milioni 232 zimeshagawiwa kwa wakulima wa West Kilimanjaro kwa ajili ya kuwapatia mitaji wezeshi kwa zaidi ya 14,000 kutoka katika vikundi 1,500 kwa ajili ya mahitaji ya malighafi na pembejeo za kilimo na mpaka sasa maombi ya Sh. milioni 132.1 yako katika hatua za mwisho za kuidhinishwa", alisema Tully.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Michelle Kilpin alisema: "Tunatoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa wakulima wadogo kupitia mawakala wetu walioko katika maeneo husika ili tuwawezesha kupata mavuno mengi katika eneo dogo, wafanye kilimo chenye tija na mbegu zinazotumika katika zao la shahiri hutolewa na kampuni yetu."

# RC ampa siku 30 DED uzio ujengwe katika kituo cha makazi ya wazee

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ametoa siku 30 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kutuma timu ya wataalamu wa ardhi kwenda katika Kituo cha Makazi ya Wazee wasiojiweza cha SUKAMAHELA kwa ajili ya kupima na kuweka mipaka ya kituo hicho.

Amesema kuweka mipaka katika kituo hicho kutasiadia kudhibiti wananchi kuvamia eneo hilo na kuanzisha shughuli za kiuchumi, yakiwamo mashamba.

Dendego alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea kituo hicho na kukabidhi zawadi mbalimbali zilizotolewa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kituo hicho. Hizo ni televisheni, friji, nguo na vyakula kwa ajili ya sikukuu ya Eid el Fitr.

Alisema kuwa baada ya mwezi mmoja, apatiwe taarifa ya utekelezaji agizo hilo, vinginevyo atachukua hatua dhidi ya watendaji ambao hawatatekeleza agizo hilo.

Alisema watendaji wanapaswa kutekeleza agizo hilo kuhakikisha wazee wanaotunzwa kwenye kituo hicho wanakaa na kupewa huduma vizuri bila kubughuziwa na mtu.

"Hawa wazee wametutumikia sana, wametufanya tuwe hapa tulipo, hivyo ni lazima tuwaheshimu, tuwalee na tuwatunze," alisisitiza.

Kuhusu tatizo la kukosekana huduma ya maji na umeme kwenye kituo hicho, Mkuu wa Mkoa aliagiza watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Singida na wa Mamlaka ya Maji waende kwenye kituo hicho na kuweka kambi ili huduma hizo muhimu zipatikane muda wote kwenye kituo hicho.

Alifafanua kuwa siku 14 zinatosha kuweka huduma za maji na umeme kwenye kituo hicho kama hatua ya kuhakikisha wazee hao wanaishi maisha yenye staha kulinganishwa na hali ilivyo kwa sasa.

Alisisitiza kuwa kupatikana huduma hizo kutasaidia ulinzi kwa wazee hao pamoja na kuwaepusha na vitendo vya kushambuliwa na wanyama wakali hasa nyakati za usiku.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, aliwataka watumishi wa serikali wanaofanya kazi kwenye kituo hicho, kufanya kazi kwa weledi, bidii na ufanisi katika kuwalinda na kutunza wazee hao ili waishi maisha mazuri na yenye furaha kama watu wengine.

Alisema kuwa wazee ni hazina na baraka, hivyo lazima wahudumiwe ipasavyo na kupatia huduma za msingi kama jamii nyingine.

Kituo cha Makazi ya Wazee Wasiojiweza cha SUKAMAHELA kilichoko wilayani Manyoni, kilianzishwa mwaka 1974 kwa ajili ya kutoa huduma za tiba kwa waathirika wa ugonjwa wa ukoma ambapo kwa sasa kinahudumia wazee kutoka mikoa ya Singida na Dodoma.

**Watendaji wanapaswa kutekeleza agizo hilo kuhakikisha wazee wanaotunzwa kwenye kituo hicho wanakaa na kupewa huduma vizuri bila kubughuziwa na mtu.**

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

## DP World yaanza kazi bandari ya Dar

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya DP World ya Dubai imeanza rasmi kazi ya kushusha na kupakia makontena kwenye bandari ya Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, ilibainisha hayo huku ikielekeza wateja wa bandari hiyo kuhusu masuala mbalimbali yakiwemo namna ya kufanya malipo kwa kampuni hiyo.

Taarifa hiyo inawaelekeza wateja na watumiaji wengine wa bandari kuhusu benki zitakazotumiwa na DP World kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mizigo yao.

Kadhalika, taarifa hiyo imeonyesha wateja kuhusu mawasiliano mbalimbali yanayotumiwa na kampuni hiyo pamoja na ofisi zitakazotumiwa na maofisa wake.

Hivi karibuni, wafanyakazi wa TPA walipewa barua kuchagua kufanya kazi na mamlaka hiyo au kuhamia DP World itakapoanza kazi.

TPA iliwataka kuchagua ama kubaki katika ajira TPA au kusitisha mikataba na kujiunga na ajira mpya katika kampuni ya DP World.

Taarifa ya TPA iliyotolewa Machi 20, mwaka huu na Mbossa, ilisema Oktoba 22, 2023 mamlaka hiyo iliingia mkataba na DP World ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kuhusu uendeshaji wa gati namba sifuri hadi tatu na gati namba nne hadi saba za bandari ya Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka 30.

"Kutokana na makubaliano hayo yanayohusisha usimamizi na uendeshaji wa maeneo tajwa, watumishi wa bandari ya Dar es Salaam, wanapaswa kuchagua kati ya kubaki TPA au kusitisha mkataba wa ajira kati yao na TPA au kusitisha mkataba wa ajira wa TPA na papo hapo kuajiriwa upya na DP World," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uongozi wa TPA ulikuwa umekamilisha mchakato wa utoaji wa elimu kwa watumishi wote walio kwenye maeneo husika.

Taarifa pia ilisema mchakato wa utoaji elimu ulianza Machi 4 hadi 19, mwaka huu, kwa lengo la kuwapa watumishi wote uelewa sahihi wa mabadiliko ya uendeshaji yanayoendelea katika bandari ya Dar es Salaam.

"Pamoja na masuala mengine, elimu hii inahusisha mabadiliko ya uendeshaji wa bandari, utaratibu wa makabidhiano, utaratibu wa mtumishi kusitisha mkataba na TPA na papo hapo kuajiriwa upya na kampuni ya DP World kwa mtumishi atakayekuwa ameamua kufanya hivyo kwa hiari yake mwenyewe bila kushurutishwa.

# Jeshi la Sudan laapa kutokabidhi serikali

**KHARTOUM,** Sudan

KIONGOZI wa kijeshi nchini Sudan, Luteni Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, amesema jeshi halitakabidhi mamlaka ya taifa hilo kwa chama chochote cha ndani au kutoka nje.

"Yeyote aliyepanga njama dhidi ya watu wa Sudan ndani na nje ya nchi hatakuwa na jukumu lolote katika uendeshaji wa siku zijazo wa nchi hii," alisema Jenerali Burhan alipokuwa akiwahutubia waumini baada ya sala ya Eid al-Fitr katika msikiti mmoja katika jimbo la Gedaref.

**Yeyote aliyepanga njama dhidi ya watu wa Sudan ndani na nje ya nchi hatakuwa na jukumu lolote katika uendeshaji wa siku zijazo wa nchi hii.**

Kulingana na shirika la habari la Suna, lilimnukuu kiongozi huyo akisisitiza kwamba kila jimbo litaendeshwa na wale tu ambao wamesimama kidete dhidi ya udhalimu na ukiukaji wa haki.

Kiongozi huyo wa kijeshi alionya kwamba hakutakuwa na mazungumzo yoyote kuhusu kurejea kwa utawala wa kidemokrasia hadi pale mzozo ulioibuka Aprili mwaka jana utakapomalizika.

Jeshi limepata uungwaji mkono kutoka kwa vyama vya Kiislamu ambavyo vilikuwa na ushawishi mkubwa wakati wa uongozi wa muda mrefu wa Omar al-Bashir ambaye aliondolewa madarakani Aprili, 2019.

Mazungumzo kati ya jeshi la Sudan na kikosi cha Rapid Support Forces yanayopatanishwa na Marekani na Saudi Arabia yalitarajiwa kuendelea katika mji wa Jeddah baada ya sikukuu ya Eid.

Katika ujumbe wa sauti kwenye akaunti yake ya mtandao wa X kwa ajili ya kuadhimisha Eid al-Fitr, kiongozi wa RSF Luteni Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, anayejulikana zaidi kama Hemedti, alisema kwamba hakuna chaguo jingine kwa wanajeshi wake isipokuwa ushindi pekee.

Hemedti pia aliahidi kumfungulia mashitaka mwanajeshi yeyote atakayefanya ukiukwaji wa haki dhidi ya raia wasio na hatia na kuviagiza vikosi vyake kutomvumilia mhalifu yeyote anayetishia utulivu wa wananchi. **BBC**



Wakimbizi wa Sudan waliokimbilia Chad kunusuru maisha yao, wakipewa msaada wa chakula hivi karibuni. **PICHA: ALLIANCE**

# Wawili wafa, 6 wajeruhiwa ajali nyingine ya basi kugonga lori

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

WATU wawili wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa baada ya basi dogo la abiria (Coaster) kugonga lori kwa nyuma, likiwa limeegeshwa pembeni mwa barabara kuu ya Dodoma- Singida.

Ajali hiyo iliyotokea eneo la Kijiji cha Kintinku, wilayani Manyoni, mkoani Singida inafanya idadi ya watu waliofariki dunia kufika 11 kwa ajali za mabasi kugonga malori kwa nyuma ambazo zimetokea mkoani Singida ndani ya siku mbili.

Ajali ya kwanza ilitokea juzi saa 11 alfajiri katika Kijiji cha Milendi, Kata ya Mgongo wilayani Iramba ikihusisha basi la kampuni ya Lugiga Express lenye namba za usajiri T 315 CXX ambayo ilisababisha vifo vya watu tisa na majeruhi 19.

Basi hilo ambalo lilikuwa likitokea Dar es Salaam kuelekea mkoani Mwanza lilipata ajali hiyo baada ya kugonga lori lenye namba za usajili T 485 DBR, mali ya kampuni ya Glenrich Transportation Limited ambalo lilikuwa limeegeshwa pembezoni mwa barabara kutokana na kuharibika.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Furaha Mwakafwila, akizungumza na gazeti hili jana alisema katika ajali hiyo, abiri mmoja ambaye hakufahamika jina lake alifariki dunia papohapo baada ya ajali kutokea.

Alisema majeruhi mwingine ambaye ni kati ya majeruhi saba wa ajali hiyo alifariki dunia wakati akipelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma (General) kutokana na hali yake kuwa mbaya.

Dk. Mwakafwila alisema majeruhi sita waliobaki walipatiwa matibabu katika Kituo cha Afya Kintinku na waliruhusiwa baada ya hali zao kuwa nzuri.

Wakati huo huo, majeruhi 11 wa ajali ya basi la Lugiga Express ambao walikuwa wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida (Mandewa) wanaendelea vizuri na matibabu ambapo mmoja kati ya hao amehamishiwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma.

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS 'LIVE' APRILI 25

**Na Saada Akida**

WATANI wa jadi katika Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, Yanga Princess na Simba Queens zitakutana katika mechi ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo itakayochezwa Aprili 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza, Simba Queens walikuwa nyumbani na waliibuka na ushindi wa mabao 3-1.**

Mchezo mwingine mkubwa ambao mashabiki wanautolea 'macho' utakuwa Aprili 29, mwaka huu kati ya Simba Queens dhidi ya mabingwa watetezi wa ligi hiyo, JKT Queens.

Ikumbukwe mechi ya mzunguko wa kwanza kati ya JKT Queens na Simba haikuchezwa kutokana na Maafande hao kushindwa kwenye uwanja rasmi uliopangwa na baada ya kuamua kubakia nyumbani kwao ( Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo).

Mabingwa hao watetezi walikatwa pointi tano na Simba Queens ilipewa pointi tatu na mabao matatu.

Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, amesema timu yake haina hofu juu ya ratiba hiyo kwa sababu wamejipanga vizuri kukabiliana na kila timu inayoshiriki ligi hiyo.

Makanya alisema wanaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiweka imara na mechi zote za mzunguko wa pili wa ligi hiyo yenye timu 10.

"Hatuna presha juu ya ratiba hiyo, tunawafahamu wapinzani wetu, makocha wanaendelea kusuka vyema kikosi chetu ili kujiweka imara, kwanza tunahitaji kushinda kila mechi iliyopo mbele yetu kabla ya kucheza na Yanga Princess pamoja na JKT Queens," alisema meneja huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, alisema kwa sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika mechi dhidi ya Baobab Queens na Amani Queens ambazo ziko jirani.

"Kwa sasa tunachaangalia hizi mechi zilizopo mbele yetu, kuna mechi mbili, tunahitaji kupata matokeo na baada ya hapo tutafanya maandalizi kuelekea mchezo wetu wa dabi," alisema kocha huyo.

Mzunguko wa pili wa ligi hiyo utaanza Aprili 15, mwaka huu.



Meneja Mkuu wa Chapa ya Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Ester Raphael (kushoto), akiwa na msanii wa bongo flava, Diamond Platnumz baada ya kutangaza tamasha la muziki litakalofanyika Aprili 26 na 27, mwaka huu jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Diamond, SBL waandaa tamasha*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa ushirikiano na msanii wa bongo flava, Diamond Platnumz wametangaza kuandaa tamasha la muziki na utamaduni litakalofanyika Aprili 26 na 27, mwaka huu kwenye viwanja vya Posta Kijitonyama, Dar es Salaam.

Mbali na Diamond Platnumz wasanii wengine watakaotoa burudani katika tamasha hilo ni Billnass, Darassa, Rosa Ree, Whozu na Casper Nyovest kutoka Afrika Kusini.

Meneja wa Chapa wa SBL, Ester Raphael, alisema kwa kushirikiana na Diamond Platnumz wanadhihirisha upendo kwa utamaduni wa Kitanzania.

Alisema Diamond anawakilisha vyema taifa letu na hivyo ni chaguo sahihi kwa tamasha hili.

"SBL na Diamond Platnumz wote wanadhihirisha kiini cha Utanzania. Ushirikiano huu unatukumbusha umoja wetu na kuonyesha kinachoifanya Tanzania kuwa ya kipekee kama ambavyo bia ya Serengeti inavyokidhi ladha zetu," Rhona Namanya, Meneja Masoko wa SBL, alisema.

Naye Diamond Platnumz, ambaye pia anajulikana kama Simba Dangote, alisema; " Nina furaha kubwa kuwa sehemu ya tamasha hili la kihistoria kusherehekea muziki na utamaduni wetu wenye thamani kubwa. Tukio hili litawakutanisha wasanii bora wa Tanzania, sanaa, na utamaduni," alisema msanii huyo.

## Kocha mpya Tabora United aanza nyodo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa kwanza akiwa na Tabora United, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Denis Goavec, ametamba ataendeleza 'moto' huo huo katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizosalia.

Kocha huyo amesema hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya Singida Fountain Gate na kuongeza anataka kuweka rekodi pia ya kushinda mechi ya Ligi Kuu tangu alipotua klabuni hapo.

Alisema anahitaji kuondoka na pointi tatu watakapoikaribisha JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

"Nadhani baada ya kucheza mechi nane hivi, tumepata ushindi wa kwanza, lakini huu umekuwa ushindi wangu wa kwanza mara tu baada ya kuingia, ina maana nimeingia na bahati, lakini bado, ile ilikuwa ni Kombe la FA, nataka nishinde mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumamosi na nyingine zinazofuata," alisema kocha huyo raia wa Ufaransa.

Tabora United iko katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 21, imebakisha michezo tisa ili ikamilishe msimu huu.

## KMKM yawaza kucheza fainali Kombe la FA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kila mwaka kutolewa mapema katika mashindano ya Kombe la ZFF (FA Cup), mara kadhaa, benchi la ufundi la KMKM limesema mpango wake mkubwa msimu huu ni kucheza hatua ya fainali ya michuano hiyo.

KMKM itashuka dimbani kuwakabili Paje Star katika hatua ya 16 bora ya michuano hiyo itakayochezwa Aprili 18, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM SC, Ame Msimu, alisema wameanza maandalizi ya michuano hiyo mapema ili kuhakikisha wanafikia malengo yao.

"Tunajipanga ili tufanye vizuri na kusonga mbele katika mechi hiyo ya hatua ya 16 bora, kwetu tunauchukulia mchezo ni mgumu katika safari ya kufikia malengo, tunataka kuona mwaka huu mpango wetu wa kufika fainali," alisema Msimu.

Aliongeza ushindani huwa mkubwa wanapokutana na klabu za madaraja ya chini dhidi ya timu ya Ligi Kuu na msimu huu hawataki kuona wanaishia hatua ya robo fainali.

## ZISIKUPITE

### TONEY AGOMBEWA SOKONI

KLABU za Arsenal na Chelsea zinamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney, 28, ambaye atagharimu hadi pauni milioni 40 msimu huu wa joto. ***(Florian Plettenberg)***

### GYOKERES KUONDOKA LISBON

WAKALA wa mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres, 25, amesema itakuwa vigumu kwa mchezaji huyo kusalia Sporting Lisbon ikiwa Kocha, Ruben Amorim, ambaye anahusishwa na Liverpool, ataondoka katika klabu hiyo. ***(A Bola)***

### FONSECA KUTUA WEST HAM

KOCHA wa Lille, Paulo Fonseca, anaongoza orodha ya wanaozingatiwa na West Ham kuchukua nafasi ya ukocha ikiwa wagonganyundo hao wataachana na David Moyes katika majira ya joto. ***(I)***

### OSIMHEN ATAJWA CHELSEA

CHELSEA inamlenga mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, msimu huu wa joto lakini klabu hiyo itahitaji kwanza kuuza wachezaji ili kupata fedha.***(Football Transfers)***

### AMKERA POCHETTINO

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, hajafurahishwa na mchezo wa fowadi wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk, 23, msimu huu na The Blues watakuwa sokoni kutafuta winga mpya msimu huu. ***(Football Insider)***

### SUMMERVILLE AGEUKA LULU

KLABU ya Bayer Leverkusen imeungana na Liverpool na Tottenham Hotspur katika harakati za kumwania winga wa Leeds United, Crysencio Summerville, mwenye umri wa miaka 22. ***(Bild via Teamtalk)***

### LUIZ KUJICHIMBIA VILLA

ASTON Villa inazidi kupata matumaini kuhusu kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Douglas Luiz, 25, atasaini mkataba mpya wa muda mrefu. ***(Talksport)***

### SUDAKOV RASMI SOKONI

KLABU ya Donetsk inajiandaa kumuuza kiungo wa kati wa Ukraine, Georgiy Sudakov, huku Liverpool, Aston Villa, Arsenal na Manchester City zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(HITC)***

### VILLA YAMTAKA DUMFRIES

MLINZI wa Inter Milan, Denzel Dumfries, 27, anaweza kulengwa na Aston Villa na klabu hiyo ya Italia itazingatia ofa ya zaidi ya euro milioni 30 kwa mchezaji huyo wa Uholanzi ambaye mkataba wake na timu hiyo ya Serie A utamalizika mwakani. ***(Calciomercato)***

### UNITED KUTEMA NYOTA 12

MANCHESTER United itawaacha wachezaji 12 wa kikosi cha kwanza wa timu hiyo ya Old Trafford katika hatua ambayo itakuwa kubwa yenye lengo la kuunda timu mpya ya klabu hiyo. ***(FourFourTwo)***

### NUBEL, BAYERN MAMBO SAFI

GOLIKIPA wa Ujerumani, Alexander Nubel, 27, anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na Bayern Munich ambao utahusisha kuendeleza mkataba wake wa mkopo na Stuttgart kwa msimu mwingine.***(Bild)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AIWEKA BARCA 'NJIA PANDA' ULAYA

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amesema Paris Saint-Germain bado ina nafasi kubwa kushinda mechi ya pili ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, licha ya timu yake kushinda mabao 3-2 katika mchezo wa kwanza uliochezwa jijini hapa juzi.

**Raphinha alifunga mabao mawili na mchezaji wa akiba, Andreas Christensen, akaongeza goli lingine kwa kichwa dakika ya 77 katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Parc des Princes.**

"PSG bado ni ina nafasi," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo. "Itakuwa ngumu sana kushinda Barcelona.

"Leo (juzi) tumecheza vizuri kwa sababu tulikuwa na umoja katika safu ya ulinzi, najivunia sana, kila

## ●●● Kocha huyo asema PSG ina nafasi ya kusonga mbele licha ya...

kitu kilifanya kazi vizuri, inabidi tuboreshe umakini katika dakika za kwanza za kipindi cha pili, tulifanikiwa kukomaa na kupona mechi ambayo ilikua ngumu sana. "

Barcelona ambao waliwashinda Napoli katika hatua ya 16 bora, wanatafuta kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu 2019 kufuatia kutolewa mfululizo kwenye hatua ya makundi.

"Natumai mizimu imekufa," alisema Xavi.

"Tumepitia miaka migumu katika Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ushindi huu unaonyesha Barca bado wako hai."

PSG walionekana kupona baada ya bao la kuongoza la Raphinha wakati Ousmane Dembélé aliposawazisha dakika ya 48 dhidi ya timu yake ya zamani.

Dakika tatu baadaye kiungo Vitinha aliiweka PSG mbele kutokana na pasi ya Fabian Ruiz katika mechi ya kusisimua ambapo Dembélé pia aligonga nguzo ya kushoto dakika chache kabla ya bao la ushindi la Christensen.

"Hatujafurahishwa na kushindwa," Kocha wa PSG, Luis Enrique, ambaye alishinda mataji matatu akiwa na Barcelona mwaka 2015, alisema.

"Mchuano wa pili utakuwa kama fainali sasa, ni lengo letu. Sina shaka tunaweza kufuzu. Naipongeza Barcelona kwa ushindi wao na uchezaji wao.

"Tungefanya vizuri zaidi na itabidi tuboreshe baadhi ya mambo kwenye mechi ya mkondo wa pili lakini bado nimeridhishwa na nilichokiona usiku wa leo (juzi).

# BRANTHWAITE HATAKI 'KELELE'




**LONDON,** England

MLINZI wa Everton, Jarrad Branthwaite, ambaye amezivutia Manchester United na Real Madrid, amesisitiza anazuia 'kelele' zinazohusu mustakabali wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amekuwa muhimu sana msimu huu, akiisaidia Toffees ambayo inapambana na janga la kushuka daraja baada ya kupunguzwa kwa pointi sita kwa kukiuka kanuni za Faida na Uendelevu za Ligi Kuu England.

Kiwango cha Branthwaite kilimfanya aitwe kwa mara ya kwanza katika kikosi cha Timu ya Taifa ya England kwa ajili ya mechi za kimataifa zilizochezwa Machi, lakini ni mustakabali wake wa muda mrefu ambao umetawala vyombo vya habari bado haujajulikana.

Hivi karibuni 90min ilifichua Manchester United na Real Madrid zinavutiwa na kipaji cha beki huyo.

Mkataba wake pale Goodison Park utaendelea hadi mwaka, 2027 baada ya masharti mapya kuongezwa Oktoba, mwaka jana na Everton wanatarajiwa kulipwa zaidi ya pauni milioni 70 ikiwa Branthwaite ataondoka.

Lakini alipoulizwa kuhusu mustakabali wake, Branthwaite alifichua amedhamiria kupuuza uvumi huo ili kuangazia kuisaidia Everton kufikia malengo yao.

"Ni lazima tu kuzuia yote nje. Nadhani kama wewe kuzingatia mambo ya nje, kupata nini unahitaji kufanya uwanjani," alisema.

"Kwangu sasa, hadi mwisho wa msimu, ninalenga tu kushinda michezo kwa klabu yangu ya Everton."

Branthwaite ana nafasi ya kujumuishwa katika kikosi cha England cha Euro 2024 msimu huu wa joto, ingawa uamuzi wa Gareth Southgate wa kutomtumia dhidi ya Brazil na Ubelgiji labda unaonyesha msimamo wake wa sasa katika mpangilio wa beki wa kati.

# Diego Simeone ajutia kupoteza nafasi



**MADRID,** Hispania

KOCHA Diego Simeone alisifu uchezaji wa Atletico Madrid katika ushindi wao wa mabao 2-1 wa mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund, lakini akasikitikia timu yake kushindwa kutumia nafasi ambazo zingewapa faida kubwa katika mchezo huo wa kwanza wa hatua ya robo fainali.

Atletico walitawala sehemu kubwa ya mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye uwanja wa nyumbani wa Metropolitano juzi usiku, huku Rodrigo de Paul akiwaweka mbele dakika ya nne naye Samuel Lino akafanya matokeo kuwa 2-0.

Antoine Griezmann na Lino walipata nafasi ya kuendeleza uongozi wao, kabla ya Dortmund kupata bao la dakika za mwisho kupitia kwa Sebastian Haller na kuwapa matumaini kuelekea katika mechi ya marudiano Jumanne ijayo nchini Ujerumani.

"Kila sare katika raundi hii imekuwa sawa: Real Madrid v Manchester City, Arsenal v Bayern na yetu pia," alisema Simeone akiiambia Movistar.

"Tuliona kwenye mchezo kati ya Manchester City na Real Madrid zaidi ya yote, ni miongoni mwa timu bora katika nane bora. Wanashangaza, kila wanapokaribia goli, wanafunga, na hiyo inaleta tofauti.

"Tulikuwa na dakika 60 au 70 nzuri sana, na ni kawaida wakati ambapo mpinzani anaweza kufanya jambo. Walifanya hivyo, na wangeweza kupata sare."

Simeone alimlinda fowadi wa Álvaro Morata, ambaye amefunga bao moja pekee tangu Januari baada ya kipindi cha kipekee cha kwanza cha msimu.

"Kuna mambo ambayo huwezi kueleza, ambayo ni ya asili," alisema Simeone katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo kumalizika.

"Alvaro alikuwa na miezi sita ya kuvutia kuanzia Julai hadi Januari. Sasa yuko katika wakati mgumu zaidi, hapati bao, lakini anafanya kazi kwa bidii na kupitia kazi hiyo, malengo yatatimia."

# Vinicius Jr hataki kuondoka Madrid

**MADRID,** Hispania

VINICIUS Jr hana nia ya kuondoka Real Madrid msimu huu wa joto licha ya ujio wa Kylian Mbappe, ripoti kutoka Hispania imesema.

Real Madrid watamwongeza Mbappe katika safu yao ya washambuliaji msimu huu wa joto kwa uhamisho wa bila malipo, na hivyo kumaliza kukaa kwa miaka sita PSG, na sasa mustakabali wa muda mrefu wa Vinicius Bernabeu umetiliwa shaka.

Bado haijabainika Mbappe atacheza nafasi gani Madrid mara tu atakapowasili lakini mantiki inaweza kupendekeza atarithi mikoba iliyoachwa na Karim Benzema.

Carlo Ancelotti amebadilisha mbinu zake msimu huu ili kufidia kuondoka kwa Benzema kwa kushtukiza mwaka jana, akiwatumia Vinicius na Rodrygo kama wachezaji wawili wa mbele huku Jude Bellingham akiwa nyuma.

Vinicius amehusishwa na uhamisho wa pauni milioni 200 kwenda PSG – kuchukua nafasi ya Mbappe - huku pia akitajwa katika rada za Liverpool huku wakifikiria kuchukua nafasi ya Mohamed Salah, ambaye anasakwa kwenye Ligi Kuu ya Saudia.

Lakini gazeti la Marca limeripoti Vinicius, wawakilishi wake na Real Madrid wenyewe hawana nia ya kuwezesha kuondoka msimu huu wa joto, na mchezaji huyo anafahamika ana furaha sana katika mji mkuu wa Hispania.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anasemekana kupenda maisha ya kila siku huko Madrid kwa sababu anahisi 'kuheshimiwa' na 'kupendwa' na wote katika klabu hiyo, na anahisi kusalia klabuni hapo itakuwa uamuzi bora zaidi wa kikazi.



## Simba, Yanga hasira Ligi Kuu Bara

INATOKA UKURASA 24

ambalo ni la Ngao ya Jamii baada ya kuwafunga Yanga penalti 3-1, katika mechi ya fainali ya michuano hiyo iliyochezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, Tanga.

"Hivi sasa Simba imebakiwa na chaguo moja au taji moja la kulipigania nalo ni la Ligi Kuu Tanzania Bara, tumepoteza mataji mengine yote ambayo yalikuwa katika mikono yetu na tulikuwa tunayapigania, taji pekee lililo mikononi mwetu ni hili.

Yapo maneno mengi, wapo wanaosema wamekata tamaa, lakini niseme bado tunayo nafasi kubwa katika ligi ili tukianguka tuwe wote pamoja na kama tukifaulu, tufaulu pamoja tufurahi wote," alisema Ahmed.

Simba inajiandaa kucheza dhidi ya Singida Black Stars (zamani Ihefu), katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida.

Aliongeza hali ya Henock Inonga imeimarika na atarejea katika kikosi huku akimtaja kipa, Aishi Manula, ndiye anabakia mchezaji atakayekuwa kuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu.

## Clement Mzize awapotezea wanaombeza

INATOKA UKURASA 24

michezo miwili iliyopita jambo lililozalisha 'maneno' juu yake, aliongeza bado hatayapa nafasi anapokuwa uwanjani.

"Mara nyingi Kocha Miguel ananiambia natakiwa kufuata maelekezo yake anayonipa mazoezi na kuhamishia uwanjani, ananiamini na nisipaniki, nisitoke mchezoni kwa sababu ya kutofanya vizuri katika mechi mbili zilizopita," alisema Mzize.

Aliongeza amefanikiwa kucheza kwa kufuata maelekezo na ataendelea kupambana na kujituma ili kuboresha kiwango chake.

"Nitajituma na kupambana kila ninapopata nafasi ya kucheza ili kuhakikisha ninafunga na kutafuta tuzo ya ufungaji bora wa michuano hiyo (Kombe la FA), sitasikiliza maneno ya nje," alisema mshambuliaji huyo.

Mzize amekuwa msaada katika safu ya washambuliaji wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga akishirikiana na nyota wengine tegemeo ambao ni Stephane Aziz Ki, Pacome Zouzoua na Maxi Nzengeli.

# SERIKALI YAAHIDI KUONGEZA NGUVU 'VITA' YA HAKIMILIKI

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewahakikishia wadau wa sekta ya utangazaji itaongeza nguvu katika kukabiliana na changamoto ya wizi wa maudhui ya televisheni unaofanyika kwa njia mbalimbali ikiwamo mitandao ili kuepusha kuporomoka kwa sekta hiyo na kulinda haki za makampuni ya utangazaji pamoja na wazalishaji wa maudhui.

Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, alisema hayo katika hafla ya kuadhimisha mafanikio ya uzalishaji wa maudhui ya kitanzania unaofanywa na MultiChoice Tanzania iliyofanyika jijini, Dar es Salaam hivi karibuni.

**Mwinjuma alisema serikali inaongeza nguvu katika kupambana na uvunjwaji wa hakimiliki na ndiyo sababu imeendelea kuiimarisha Ofisi ya Hakimiliki nchini (COSOTA), kwa kuiongezea vitendea kazi.**

"Tutaendelea kushirikiana na mamlaka nyingine katika kuhakikisha suala hili linashughulikiwa kwa uzito unaostahili na katika hili tutahakikisha tunalishughulikia kwa muktadha mpana kwa sababu suala hili haliwaathiri wazalishaji wa maudhui tu, bali hata msanii mmoja mmoja," alisema kiongozi huyo.

Aliipongeza MultiChoice Tanzania kwa uwekezaji mkubwa inayofanya katika uzalishaji wa maudhui ya ndani hususani filamu huku akiutaja uwekezaji huo kama chachu kubwa ya ukuaji wa tasnia ya filamu hapa nchini.

Alisema kitendo cha MultiChoice kuwa na chaneli maalum za Maisha Magic Poa na Maisha Magic Bongo ambazo hurusha maudhui ya Kitanzania, kumeifanya tasnia ya filamu kukua hapa nchini na kuongeza mchango wake katika kutoa ajira na kukuza uchumi.

Naye Mwenyekiti wa MultiChoice Tanzania, Balozi Ami Mpungwe, alisema kampuni hiyo imejipanga kuendelea kuwekeza katika uzalishaji wa maudhui ya kitanzania na ili kuhakikisha tasnia ya filamu inakua na inatoa mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi.



Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma (wa pili kulia), akiingia katika sherehe ya kuadhimisha mafanikio ya uzalishaji wa maudhui ya Kitanzania iliyoandaliwa na Kampuni ya MultiChoice Tanzania. Kushoto ni Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Balozi Ami Mpungwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# *Azam, Namungo mechi ya kisasi*

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Azam FC umesema licha ya kuhitaji pointi tatu ili kumaliza ligi ikiwa katika nafasi mbili za juu, lengo lao lingine kubwa ni kulipa kisasi dhidi ya Namungo kutokana na kupoteza mechi ya nyumbani ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Oktoba 27, mwaka jana Azam ikiwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ilikubali kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Namungo.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano wa Azam, Thabit Zacharia, alisema moja kati ya mechi muhimu zaidi msimu huu kwao katika Ligi Kuu Bara ni dhidi ya Namungo itakayochezwa keshokutwa mkoani Lindi.

Zaka alisema mbali na kuhitaji pointi tatu kutokana na vita kali iliyopo juu kati yao na vigogo, Simba na Yanga, lakini wanahitaji kulipiza kisasi kwa sababu hawaelewi sababu iliyofanya wakafungwa katika mechi wa kwanza.

"Ni mchezo muhimu kwetu japo tupo juu ya Simba, lakini tuko huko kwa sababu tumecheza michezo mingi zaidi, hivyo hatutakiwi kupoteza michezo iliyobaki, hatutakiwi kuangusha pointi zaidi kwa sababu kuna wenzetu tumewazidi lakini wana michezo michache.

Halafu kisasi ni haki, tunakwenda kulipiza kisasi kwa sababu mchezo wa kwanza walitufunga hapa kwetu Azam Complex," alisema Zaka Zakazi.

Azam FC inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa nafasi ya pili kwenye msimamo, ikiwa na pointi 47, nyumba ya Yanga inayoongoza kwa pointi 52 na juu ya Simba iliyo nafasi ya tatu yenye pointi 45.

Hata hivyo, Azam imecheza mechi mbili zaidi ukilinganisha na Simba, ikiwa imeshuka dimbani michezo 21, Wekundu wa Msimbazi wakicheza mechi 19 mpaka sasa.

# Michezo


Ijumaa Aprili 12, 2024

Nipashe




Vinicius Jr hataki kuondoka Real

UKURASA 22



Abdelhak Benchikha

Miguel Gamondi

## Mzize awapotezea wote wanaombeza

**Na Saada Akida**



MSHAMBULIAJI wa Yanga, Clement Mzize, amesema hatasikiliza 'kelele' za mashabiki na badala yake ataendelea kufuata maelekezo anayopewa na kocha wake, Miguel Gamondi, ili kuisaidia timu yao kupata matokeo mazuri katika michezo mbalimbali.

Mzize ametoa kauli hiyo baada ya kuisaida Yanga kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma juzi usiku.

Bao lingine la Yanga katika mechi hiyo lilipachikwa na beki wa Dodoma Jiji, Emmanuel Martin, ambaye alijifunga.

Akizungumza na Nipashe jana, Mzize alisema anafurahi kuona Gamondi anampa nafasi ya kucheza na anamwamini hali inayomtengenezea kujiamini na kufanya vizuri.

Mzize alisema licha ya kutofanya vizuri katika

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba, Yanga hasira Ligi Kuu

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

●●● Kila timu inajipanga kuvuna pointi tatu muhimu katika kila mechi ili...

BAADA ya kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe ya FA, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kwa sasa anajipanga kuhakikisha anaondoka na pointi tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountain Gate FC itakayochezwa keshokutwa.

**Kwa upande wa Simba iliyoondolewa katika michuano ya Kombe la FA na Mashujaa FC ya Kigoma hapo juzi, pia imetangaza 'vita' kwa kusema inaelekeza akili na mipango yake yote kuhakikisha inafanya vizuri katika mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobakia.**

Yanga imesonga mbele katika michuano ya Kombe la FA baada ya kuifunga Dodoma Jiji FC mabao 2-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma huku Simba ikitupwa nje ya mashindano hayo kwa kufungwa penalti 6-5 na Mashujaa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gamondi, alisema ugumu waliokutana nao katika michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns umewasaidia kupata matokeo chanya walipokutana na Dodoma Jiji FC.

Gamondi alisema sasa anageuzia nguvu zake kuhakikisha wanavuna pointi tatu katika mchezo huo wa Ligi Kuu ili kuendelea kujiimarisha kwenye vita ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.

"Nimefurahi kupata matokeo chanya katika mchezo mgumu dhidi ya Dodoma Jiji FC na kusonga mbele, haikuwa mechi rahisi kutokana na ugumu wa wapinzani wetu walivyokuwa," alisema Gamondi.

Aliongeza Yanga ilikuwa na kipindi kigumu kwa dakika zote 90 kutokana na Dodoma Jiji kuwa imara na hali hiyo ilitokana na kikosi chao kuundwa na idadi kubwa ya wachezaji vijana lakini walifanikiwa kucheza kwenye mipango yao na kupata ushindi.

"Ni mechi nzuri, niwapongeze wachezaji wangu, lakini bado tuna kazi nyingi mbele, kuna mechi ya ligi tunaenda kucheza, muda ni mfupi wa maandalizi, tunatakiwa kuwa makini kwa kila mechi ili kupata matokeo mazuri hasa katika ligi kwa lengo la kutetea taji letu," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Kuhusu kurejea, Khalid Aucho, alisema ameanza kumpa nafasi ya kucheza dakika chache kiungo huyo baada ya kupona majeraha, amefanya vizuri katika mchezo wa juzi.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema hali ya Pacome Zouzoua ni nzuri na anatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi cha mchezo dhidi ya watani wa jadi Simba utakaochezwa Aprili 20, mwaka huu.

Kamwe alisema Aucho amepona na tayari aneanza kucheza na hivi karibuni wanatarajia kumuona urejeo wa Pacome wakitarajia kumuona uwanjani Aprili 20 mechi dhidi ya Simba.

"Pacome yupo na Aprili 20, mwaka huu katika mchezo wetu dhidi ya Simba atakuwa sehemu ya kikosi baada ya kupona na kuanza mazoezi ya ushindani na kugongana," alisema Kamwe.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya kutupwa nje katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la FA, sasa viongozi, benchi la ufundi na wachezaji 'wanakusanya' nguvu kwa ajili ya kupambana ili kupata ubingwa wa Bara.

Hata hivyo Simba tayari inashikilia taji moja msimu huu

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >